**SERIKALI** yatumia mamilioni ununuzi vifaa wanafunzi wa uhitaji maalum

UKURASA 2



**JAJI:** Mawaziri walipotoshwa muungano Twiga, Tanga Cement

UKURASA 3


Nipashe Spotika
WINNERS 2023
MAKOCHA WA4 WALIOSHINDA KOMBE LA FA MARA NYINGI
ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Juni 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581332

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## RIPOTI YA UCHUNGUZI

# DAR HATARINI

**DAMPO** tegemeo lajaa,'madudu' watendaji, mpakuataka aambulia 'buku' kwa siku... *Endelea ukurasa 8*



Wafanyakazi binafsi wanaotafuta riziki katika dampo la Pugu Kinyamwezi wakiwa wamekaa kwenye gari bovu mahali hapo palipozingirwa na taka. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Dk. Slaa ashtuka kasi usajili wa vyama vipya vya siasa



**ADAI** ni mbinu kudhibiti upinzani 2025, ACT-Wazalendo yataka Sheria ya Madini imulikwe... *Endelea Uk. 2 & 7*

## Mwinyi akemea wanachama wa CCM kutukana viongozi wao

UKURASA 17


**MICHEZO** **YANGA HAOO IKULU** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Serikali yatumia mil. 300/- vifaa, bima afya wanafunzi wenye uhitaji

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, amesema zaidi ya Sh. milioni 300 zimetumika kwenye ugawaji wa vifaa, bima za afya na ujenzi wa mabweni kwa wanafunzi wenye uhitaji.

Mkenda aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya ugawaji wa vifaa hivyo iliyofanyika katika Shule ya Msingi ya Uhuru Mchanganyiko, ambavyo pamoja na bima ya afya vimegharimu Sh. 334, 148, 800.

"Nitafanya matukio makubwa matatu usambazaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa saidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaosoma katika vyuo vikuu nchini," alisema Mkenda.

Alisema vifaa hivyo vinakusudiwa kutatua tatizo la uhaba wa vifaa katika vyuo vikuu na kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wasioona, wenye ualbino, uoni hafifu, viziwi na wenye ulemavu wa viungo.

"Nitazindua mabweni mawili maalum yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 100 wakiwamo wasichana 50 na wavulana 50 wenye usonji na ulemavu wa akili," alisema.

Alisema mabweni hayo yatasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa akili na usonji kukaa na kutulia shuleni kwa lengo la kujifunza kiufasaha.

Kadhalika, mabweni hayo yatawaondolea wazazi adha ya kuwapeleka na kuwarudisha nyumbani, watabaki nyumbani wakiendelea na shughuli za ujenzi wa uchumi wa taifa.

Aidha, alisema itawasaidia wanafunzi hao kulindwa na vitendo vya kikatili vinavyoweza kuwapata wanapokuwa njiani.

Alisema mabweni hayo yatasaidia wanafunzi hao kuinua kiwango cha ufaulu na kurahisisha huduma za uchechemuzi na utengamao kwa kuwa walimu na walezi watapata muda mzuri wa kutimiza malengo yao.

Aidha, atagawa bima za afya kwa wanafunzi 122 wenye mahitaji maalum kwa wasichana 72 na wavulana 50 waliofanyiwa upembuzi yakinifu na kubaini ni wanafunzi wenye ulemavu wa kiwango cha juu na wengine wana changamoto ya magonjwa ya kudumu kwa kushindwa kuhudhuria kliniki kama madaktari walivyowashauri na wengine kukosa dawa ambazo wanatakiwa kutumia kwa kuwa wanatoka katika familia zenye kipato cha chini.

Mkenda alisema bima za afya zitasaidia kuimarisha afya, zao, mahudhurio shuleni na kuongeza kiwango cha ufaulu.

Alisema mojawapo ya jukumu la wizara yake ni kuimarisha utoaji wa elimu maalum na jumuishi kwa kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo ili kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kupata idadi kubwa ya Watanzania waliyoelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia kufikia malengo ya maendeleo ya taifa bila kujali tofauti zao.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau katika elimu na mafunzo, imeweka mkazo kuhakikisha uwapo wa miundombinu rafiki, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na walimu wenye sifa stahiki.

Aidha, lengo mojawapo la mapitio hayo ni kupitia na kuhakiki vikwazo vyote vinavyowakabili wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuakisi mahitaji ya sasa kwa lengo la kurahisisha mchakato wa kujifunza kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.




Wanafunzi wenye mahitaji maalum wakifurahia baada ya kugawiwa Bima ya Afya na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Slaa ashtukia kasi usajili wa vyama vipya vya siasa

**Na Enock Charles**

BALOZI mstaafu wa Tanzania nchini Sweden, Dk. Wilbrod Slaa ameshangazwa na kasi ya usajili wa vyama vipya vya siasa, akidai lengo ni kuugawa upinzani na kuua demokrasia nchini, hasa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Dk. Slaa ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alitoa kauli hiyo katika mazungumzo maalum na Nipashe nyumbani kwake Mbweni mkoani Dar es Salaam wiki iliyopita.

Alisema kwa uzoefu wake katika siasa, baadhi ya vyama vimekuwa vikitumika wakati wa uchaguzi tu, ili kuhalalisha matokeo ya uchaguzi huo na baada ya hapo hupotea.

"Hebu tazama mwaka 2020. Mimi nilikuwa nje lakini nilikuwa ninafuatilia. Vyama 14 vilijitokeza vikasema uchaguzi ulikwenda vizuri na umefanyika kwa haki. Kumbuka hata Mobutu Seseseko (aliyewahi kuwa kiongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) aliunda vyama 2,000, ili kumsaidia yeye kushinda kila wakati uchaguzi.

"Hivi karibuni Tanzania tumetangaziwa kuna maombi mapya 18 ya vyama kusajiliwa. Kumbuka kuna vile 20 vilivyopo. Ninajua lengo ni uchaguzi wa mwaka 2025. Huu ni... (alitamka neno kali).Tanzania kwa rasilimali ilizonazo, inapaswa kuwa kinara kwa Afrika nzima, lakini tunaiua kwa sababu ya kuua demokrasia.

"Kama hamjui, ninawaambia leo - demokrasia ina mchango mkubwa sana katika kuleta maendeleo ya nchi. Unaweza kusema asilimia 80 ya maendeleo ya nchi yanaletwa na nchi kuwa na demokrasia kwa sababu watu watachangia mawazo.

"Maendeleo yanayopatikana katika nchi ya kidemokrasia yanakuwa ni ya wananchi wote wakati katika nchi zisizo na demokrasia yanakuwa ni ya watu wachache, ukikuta nchi ni ya kidikteta na ina maendeleo, nenda ukaangalie upande wa pili nani anamiliki zile mali," alifafanua.

Dk. Slaa alisema demokrasia ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi, hasa ustawi wa jamii na matumizi ya rasilimali za nchi, hivyo ukishakosa demokrasia hayo mambo yote unapaswa kuyasahau.

Mwezi uliopita Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, alieleza kuwa ameshapokea maombi ya kuanzishwa vyama 18 na kabla ya maombi hayo, tovuti rasmi ya ofisi hiyo ilikuwa na idadi ya vyama 20 vyenye usajili wa kudumu, hivyo nchi itakuwa na vyama 38 ikiwa maombi hayo yatakubaliwa.

"Tulikuwa na maombi 17, lakini juzi tumepata ombi lingine la chama kimoja, hadi sasa vyama sita katika maombi hayo ndivyo vimekidhi masharti ya kupata usajili wa muda," alisema Jaji Mutungi.

Akinukuliwa na chombo kimojawapo cha habari nchini, Jaji Mutungi alisema kuwa baada ya kukidhi sifa hizo baadhi ya vyama hivyo, vitaingizwa katika mpango wa bajeti kwa ajili ya uhakiki wa wanachama wake kabla ya usajili.

Mtazamo wa Dk. Slaa katika hilo ni kwamba vyama vingi vinavyosajiliwa havilengi katika majukumu ya msingi ya kuwatetea wananchi au kuwa na uwakilishi, ikiwamo wabunge na madiwani, bali hutumika kupambana na vyama vilivyoimarika vya upinzani, ili kuwachanganya wananchi na kuwapoteza ari ya kuunga mkono upinzani.


**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI/MAOMBI MADOGO/RUFAA NA. 173 MWAKA 2023**

**DANIEL RAPHAEL NTABINDI.................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SAID MOHAMED NASORO.............MJIBU MAOMBI / WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: SAID MOHAMED NASORO**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 6 Mwezi wa 6 Mwaka 2023 saa 03:00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mhe. S. Kanyerinyeri Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo hiyo bila kukosa. Unatakiwa/Mnatakiwa ufike/mfike wewe mwenyewe/ninyi wenyewe, au Wakili wako/wenu/mwakilishi wako/wenu pasipo kukosa na ulete/mlete utetezi wako/wenu ndani ya siku ishirini na moja (21) toka tarehe ya kupokea kuitwa shaurini.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri / Muhuri wa Baraza hii leo tarehe 25 Mwezi 05 Mwaka 2023.

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA, KANDA YA BUKOBA**

**MAOMBI NA. 18/2023**

**LAMECK KIULA NA WENZAKE 4.......................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JAMBO BUKOBA**
**CLEMENCE MULOKOZI.............................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**Kwa JAMBO BUKOBA**

**CLEMENCE MULOKOZI (POPOTE MLIPO)**

Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la rufaa tajwa juu limepangwa kusikilizwa tarehe 06 Mwezi Juni Mwaka 2023 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mh. Jaji K.R. MTEULE, Mahakama Kuu, kanda ya Bukoba. Kwa hiyo, unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutohudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo hii tarehe 01 mwezi Juni mwaka 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
BUKOBA

**KUPOTEA KWA CHETI**



**REVOCATUS .V. FIVAWO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0113-0026** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya **MAFINGA SEMINARY** mwaka 2005. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/186247/2023**

# Jaji asema mawaziri walipotoshwa muunganiko Twiga, Tanga Cement

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASHERIA mkongwe nchini Jaji mstaafu Thomas Mihayo, amesema wanasheria waliipotosha serikali na mawaziri kuhusu kuendelea na mchakato wa kampuni ya Saruji ya Twiga kununua hisa za Tanga Cement wakati mahakama ilizuia kuwapo kwa muunganiko wa kampuni hizo.

Amesisitiza kuwa Baraza la Ushindani wa Biashara (FCT), lilishatoa uamuzi wa kuzuia muunganiko wa kampuni hizo baada ya wadau waliopinga suala hilo kufungua shauri na hatimaye kutolewa zuio. Akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake, Oysterbay, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Jaji Mihayo alisema baada ya kupitia uamuzi wa kisheria uliotolewa, ameshangazwa na hatua ya serikali ya kuendelea na mchakato ilhali ulishazuiwa. "Mahakama ikishaamua jambo, liwe zuri au baya, linapaswa kuheshimiwa. Kwenda kinyume cha uamuzi wa mahakama ni kuidharau mahakama. Katika suala hili la muunganiko wa Twiga na Tanga Cement mahakama ilishatoa uamuzi kwamba jambo hilo halipaswi kuendelea.

"Kwa mantiki hiyo, serikali kupitia FCC (Tume ya Ushindani), haikupaswa kwenda kinyume bali kuheshimu. Kama ilikuwa haijaridhika, kwa mujibu wa FCA (Sheria ya Ushindani), ilipaswa kuiomba FCT kufanya marejeo ya jambo hilo badala ya kuendelea. Hii ni kuidharau mahakama," alisema Jaji Mihayo huku akibainisha kuwa ni mtazamo wake binafsi kama mwanasheria.

Wakati wa majumuishi ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Waziri wa wizara hiyo, Dk. Asharu Kijaji, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Patrobas Katambi, walisimama bungeni na kutetea uamuzi wa kuendelea na mchakato huo huku wakibainisha kwamba serikali haijavunja sheria.

Dk. Kijaji na Dk. Nchemba walisema serikali iliamua kuendelea na mchakato kwa kuwa mazingira ya awali kwa maana ya soko, yalikuwa yamebadilika na kwamba hakuna na zuio katika mchakato mpya bali ile wa kwanza.

Kutokana na hoja hizo, Jaji Mihayo alisema hata kama mazingira yalikuwa yamebadilika suala hilo lilikuwa limezuiwa bila masharti yoyote, hivyo sheria imekiukwa na amri ya mahakama imedharauliwa. Jaji Mihayo alisema kuwapo kwa jambo kama hilo la kutotii uamuzi au amri ya mahakama katika mchi inayofuata utawala wa sheria ni hatari kwa maslahi ya taifa na hata maendeleo kwa ujumla. Alisema suala hilo halileti picha nzuri katika utawala wa sheria.

FCC ilitangaza muunganiko wa kampuni kupitia Scancem International DA ambayo ni sehemu ya Heilderberg Cement inayomiliki Twiga Cement na Tanga Cement, jambo ambalo lilipingwa na lilipingwa FCT na wadau wa saruji ambao ni kampuni ya Saruji ya Chalinze, Chama cha Kutetea Haki za Watumiaji wa Bidhaa na Peter Heller kwamba kunaweza kutokea athari katika soko la saruji.

Walisema iwapo Twiga itaruhusiwa kununua hisa za Tanga Cement, kuna uwezekano wa kuwapo na ukiritimba katika soko kwa kuwa Twiga Cement kupitia muunganiko huo, itakuwa na zaidi ya asilimia 68 katika soko. Hali hiyo, walisema inaweza kusababisha upangaji wa bei, hivyo watumiaji wa bidhaa kushindwa kumudu gharama.

FCT ilikubali maombi hayo na kutoa uamuzi kwamba mchakato huo unazuiwa, hivyo hakuna chochote kinachopaswa kuendelea lakini baadaye FCC ilitangaza upya mchakato huo na kuipa Twiga Cement nafasi ya kununua hisa kama mwekezaji ndani ya Tanga Cement.

Kutokana na hatua hiyo, wadau wanaopinga ununuzi huo, waliwasilisha maombi kutaka FCT kukazia hukumu iliyotoa juu ya katazo la kuendelea kwa mchakato huo. Wadau hao walisema kitendo cha FCC kuendelea na mchakato huo ilhali kuna zuio la kufanyika kwa jambo hilo, ni kinyume cha sheria zinazosimamia masuala ya miunganiko ya kampuni kwa kuwa suala hilo lilishasimamishwa.

Wakili Mkuu wa Kampuni ya Mawakili ya MSL Attorneys wanao watetea wadau hao, Melkisedech Lutema, akizungumza hivi karibuni baada ya kuendelea kwa mchakato huo, alisema kitendo cha FCC kuendelea na mchakato wakati kuna uamuzi wa kisheria kuzuia suala hilo, ni ukiukwaji mkubwa wa kisheria.

"Ni muhimu ikaeleweka kuwa uamuzi uwe sawa au si sawa na hakuna mtu aliyeupinga ni lazima uheshimiwe. Kwa hiyo mtu yeyote anayeendelea anakiuka sheria na anapaswa kuchukuliwa hatua. Kwa hili tumeiomba FCT kukazia hukumu ili uvunjaji huu wa sheria usiendelee," alisema Lutema.

# Mwigulu atoa kauli kuadimika kwa dola

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA



WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (pichani), amesema licha ya nchi ya Marekani kuja na sera ya kupunguza dola katika mzunguko, Tanzania bado ina unafuu kwa kuwa haijapata athari kubwa kulinganisha na nchi zingine kutokana na mikakati iliyowekwa na serikali.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa harambe ya kuchangia ujenzi wa shule mbili za sekondari za Kiomboi na Kititimo iliyoandaliwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Kati-Singida.

Waziri huyo alisema hatua ya Marekani na mataifa mengine makubwa kuja na sera hiyo ya kupunguza dola inayotumika kama sarafu ya kubadilishana katika biashara imefanya mazingira magumu kwa nchi zinazoendelea na zilizoendelea kwa kuwa bidhaa nyingi zinaagizwa kwa kutumia dola.

"Tunaona mambo kama vile ni magumu, lakini Tanzania tukijilinganisha na nchi zingine bado tuna unafuu na hata tukikutana mawaziri wa fedha, mimi ninaombwa kupiga picha nyingi sana kwa sababu ya hali ya uchumi ilivyo nzuri katika nchi yetu," alisema.

Dk. Mwigulu alisema bado kuna mambo ya msingi ambayo nchi inapitia kama ya kupambana na tatizo la umaskini na kukosekana kwa ajira kwa vijana nchini.

Alisema kutokana na changamoto hizo, serikali imeanzisha sera ya kuwekeza katika shughuli za uzalishaji ambazo ndio jawabu la kuwaondoa Watanzania katika umaskini na kukosekana kwa ajira kwa vijana.

Dk. Mwigulu aliongeza kuwa katika kukabiliana na changamoto ya uzalishaji duni, Rais Samia Suluhu Hassan amepandisha bajeti ya kilimo mara nne, ili kupeleka miundombinu ya umwagiliaji, ili kuongeza uzalishaji wa mazao. Hilo litawafanya wananchi kuvuna mazao kwa wingi na hivyo kuondokana na umaskini.

"Ni lazima tuipeleke nguvu kazi kazini ili iwe kazini kuongeza kipato cha mtu mmoja kwani shughuli za uzalishaji ndizo zinazokuza kipato cha mtu mmoja mmoja," alisema.

Dk. Mwigulu alisema serikali inaunga mkono jitihada zinazofanywa na taasisi za kidini katika kusaidiana na serikali katika uwekezaji katika sekta ya elimu na afya.

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kati-Singida, Dk. Syprian Hilinti, alisema katika awamu ya kwanza ya mradi huo zinahitajika Sh.milioni 500.

Aliushukuru serikali kwa kuwa na uhusiano mzuri na taasisi za dini na kuahidi kuwa wataendelea kumwombea Rais Samia.

Dola imeendelea kuadimika katika maeneo mbalimbali duniani, hali inayosababisha changamoto katika matumizi yanayohitaji sarafu hiyo ikiwamo ununuzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi.




# MATANGAZO

### HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

**Namba ya Zabuni** LGA/159/2023/2024/NC/ 06

*Kwa ajili ya utoaji wa huduma ya: HUDUMA YA KUPAKIA, NA KUSHUSHA MIZIGO MIDOGO MIDOGO YA ABIRIA (PASSENGERS) KATIKA STENDI YA NYAMHONGOLO KWA KUTUMIA MATOROLI YA MKONO (WHEEL BARROW).*

## MWALIKO WA ZABUNI

***Tarehe 05/06/2023***

1. Mwaliko huu wa Zabuni ya ushindani wa kitaifa unatokana na Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa Mwaka 2023/2024.

2. Serikali ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za ***HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA*** katika mwaka wa fedha **2023/2024**. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao unatolewa katika huu Mwaliko wa Zabuni (MZ).

3. Unakaribishwa kuwasilisha Zabuni kwa ajili ya utoaji huduma kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika **Sehemu ya Pili.**

4. Zabuni zote zijazwe kikamilifu kwa kuainisha Namba ya Zabuni ***LGA/159/2022/2023/NC/06*** HUDUMA YA KUPAKIA, NA KUSHUSHA MIZIGO MIDOGO MIDOGO YA ABIRIA (PASSENGERS) KATIKA STENDI YA NYAMHONGOLO KWA KUTUMIA MATOROLI YA MKONO (WHEEL BARROW).na kuiwasilisha kwa KATIBU WA BODI YA ZABUNI MANISPAA YA ILEMELA S.L.P 735 ILEMELA MWANZA.

5. **Mwisho wa kupokea maombi ni 19/06/2023 saa 6.00 mchana. Maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 6.00 mchana hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016..**

6. Maombi ya zabuni yatalipiwa kiasi cha shilingi 100,000 fedha hizi hazitarudishwa. Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Malipo kwa njia ya kielectroniki hayatakubaliwa.Maombi yote ya ambatishwe na picha mbili za passpoti size, za hivi karibuni.

7. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa njia ya kieletroniki hazitapokelewa.

8. Waombaji walio ndani ya pango watapewa kipaumbele.

***Mhandisi Modest J. Apolinary***
***Mkurugenzi***
***Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela***

### HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

***Tarehe 05/06/2023***

## TANGAZO LA ZABUNI

**USOMBAJI NA USAFISHAJI WA TAKA NGUMU KUTOKA KWENYE VITUO VYA KUKUSANYIA TAKA VILIVYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA KWENDA DAMPO BUHONGWA AU UTAKAPOELEKEZWA NA HALMASHAURI.**

**ITAHUSISHA KATA ZA NYASAKA, KISEKE, BUSWELU, NYAMHONGOLO KAHAMA, BUGOGWA NA SHIBULA.**

**ZABUNI Na. LGA/159/2023/2024/NC/03-I**

1. Mwaliko huu wa Zabuni unatokana na Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya **Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela** kwa Mwaka **2023/2024** wa fedha.

2. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anawatangazia Wananchi/Kampuni/Kikundi/Ushirika au yeyote mwenye sifa zinazohitajika mnakaribishwa kuleta maombi yenu, kwa ajili ya **USOMBAJI NA USAFIRISHAJI WA TAKA NGUMU KUTOKA KWENYE VITUO VYA KUKUSANYIA TAKA VILIVYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA KWENDA DAMPO LA BUHONGWA AU UTAKAPOELEKEZWA NA HALMASHAURI, ITAHUSISHA KATA ZA KATA ZA NYASAKA, KISEKE, BUSWELU, NYAMHONGOLO KAHAMA, BUGOGWA NA SHIBULA.**

**MAELEZO KWA WAOMBAJI:-**

1. Muombaji lazima awe na leseni hai kwa ajili ya Utoaji wa huduma ya usafi wa mazingira, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi (TIN), usajili wa kampuni, kama amesajiliwa kwenye VAT basi aonyeshe usajili wa VAT, Uhalali wa kisheria kusaini nyaraka (Power of Attorney).

2. Dhamana kwa muombaji ni dhamana ya zabuni kwa ahadi (Bid securing declaration)

3. Maombi yote yatumwe kwa **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, S.L.P 735 – MWANZA.**

4. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri, asiwe na historia ya kusababisha migogoro ya aina yeyote.

5. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha na vifaa vya kukusanyia taka ngumu na ahakikishe kwamba vituo vyote vya kukusanyia taka ngumu ni visafi kipindi chote cha muda wa mkataba.

6. **Mwisho wa kupokea maombi ni 19/06/2023 saa 6.00 mchana, Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.**

7. Ada ya maombi ya zabuni ni shilingi 100,000, fedha ambazo hazitarudishwa. Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni.Maombi yote yaambatishwe na picha mbili za passpoti size za hivi karibuni.

***MHANDISI MODEST J APOLINARY***
***MKURUGENZI WA MANISPAA***
***HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA***

# MATANGAZO

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

## MWALIKO WA ZABUNI

***Tarehe 05/6/2023***

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anawatangazia wananchi wenye sifa na wafanyabiashara wote, zabuni kwa ajili ya ya utoaji wa huduma ya **Ulinzi katika Kituo cha Mabasi na Maegesho ya Maroli Nyamhongolo** Namba ya Zabuni: **LGA/159/2023/24/NC/02**

1. Mwaliko huu wa Zabuni ya ushindani wa kitaifa unatokana na Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya **Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela** kwa Mwaka **2023/2024.**

2. Serikali ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za **Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela** katika mwaka wa fedha **2023/2024.** Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao utatolewa katika huu Mwaliko wa Zabuni (MZ).

3. Unakaribishwa kuwasilisha Zabuni (Bei) kwa ajili ya utoaji wa huduma kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika **Sehemu ya Pili.**

4. Zabuni zote zijazwe kikamilifu kwa kuainisha Namba ya Zabuni LGA/159/2023/24/NC/02- **Ulinzi katika Kituo cha Mabasi na Maegesho ya Malori Nyamhongolo** na kuiwasilisha katika **Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni - Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.**

5. **Mwisho wa kupokea maombi ni 19/06/2023 saa 6.00 mchana. Maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 6.00 mchana hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.**

6. Maombi ya zabuni yatalipiwa kiasi cha shilingi 100,000 fedha hizi hazitarudishwa. Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Malipo kwa njia ya kielectroniki hayatakubaliwa.Maombi yote ya ambatishwe na picha mbili za passpoti size, za hivi karibuni.

7. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa njia ya kieletroniki hazitapokelewa.

8. Waombaji walio ndani ya pango watapewa kipaumbele.

***Mhandisi Modest J. Apolinary***
***Mkurugenzi***
***Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela***

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

## TANGAZO LA ZABUNI

***Tarehe 05/06/2023***

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anawatangazia wananchi wenye sifa kwa ajili ya utoaji wa Huduma ya usafi katika Kituo cha Mabasi na Maegesho ya Maroli Nyamhongolo Zabuni Na; **LGA/159/2023/2024/NC/09.**

**MAELEZO KWA WAOMBAJI**

1. Serikali ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika mwaka wa fedha 2023/2024. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao utatolewa katika huu Mwaliko wa Zabuni(MZ).

2. Unakaribishwa kuwasilisha Zabuni kwa ajili ya utoaji wa huduma kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya Pili.

3. Zabuni zote zijazwe kikamilifu kwa kuainisha Namba ya Zabuni **LGA/159/2021/22/NC/09** Huduma ya usafi katika Kituo cha Mabasi na Maegesho ya Malori Nyamhongolo na kuiwasilisha kwa **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, S.L.P 735 - MWANZA.**

4. Mwombaji awasilishe zabuni halisi na nakala mbili, endapo maelezo ya halisi na nakala yatatofautiana maelezo yaliyopo kwenye nyaraka halisi ndio yatatumika kwenye tathmini.

5. Maombi ya zabuni yatalipiwa kiasi cha shilingi 100,000.00 fedha hizi hazitarudishwa. Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni. Malipo kwa njia ya kielectroniki hayatakubaliwa.Maombi yote ya ambatishwe na picha mbili za passpoti size, za hivi karibuni.

6. Muombaji lazima awe na leseni hai kwa biashara husika anayokusudia kuitekeleza, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi (TIN), usajili wa kampuni, kama amesajiliwa kwenye VAT basi aonyeshe usajili wa VAT, Uhalali wa kisheria kusaini nyaraka (Power of Attorney).

7. Dhamana kwa muombaji ni dhamana ya zabuni kwa ahadi (Bid securing declaration).

8. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa njia ya kieletroniki hazitapokelewa.

9. Mwisho wa kupokea maombi ni 19/06/2023 saa 6.00 mchana. Maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 6.00 mchana hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.

***MODEST J. APOLINARY***
***MKURUGENZI WA MANISPAA***
***HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA***

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Yanga inastahili pongezi kuiwakilisha vyema nchi

**WAWAKILISHI** wa Tanzania juzi walihitimisha safari yao ya kuwania kutwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika baada ya mchezo wa pili wa fainali uliochezwa kwenye Jiji la Algers, nchini Algeria.

Yanga licha ya kushinda kwa bao 1-0 ugenini bado matokeo hayo hayakuweza kuwapa nafasi ya kutangazwa mabingwa wa michuano hiyo kwa mara ya kwanza baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa Mei 28 jijini Dar es Salaam kufungwa mabao 2-1.

Ni kweli Yanga haijafanikiwa kutwaa ubingwa huo, lakini imeonyesha ushindani wa hali ya juu na kuitangaza nchi kwenye soka la Afrika.

Wapo watakaowabeza Yanga baada ya kushindwa kutwaa ubingwa huo, lakini ukiwa mpenzi wa soka huwezi kubeza mafanikio waliyofikia Yanga msimu huu kwenye mashindano ya kimataifa.

Awali Yanga waliweka wazi malengo yao kwenye mashindano ya kimataifa hususani kwenye michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho baada ya kuondolewa mapema kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kupitia kwa Rais wake, Injinia Hersi Saidi, Yanga walikuwa na malengo ya angalau kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo, lakini kujituma kwao na ubora wa kikosi chao wamefanikiwa kuvuka malengo yao na kucheza fainali ya michuano hiyo.

Tunafahamu upo ubishani na utani wa jadi, lakini Yanga wanastahili pongezi nyingi baada ya kufika fainali na kuonesha ushindani mkubwa dhidi ya klabu kubwa ya USM Algers.

Kile walichokifanya Yanga kila mpenzi wa soka katika nchi hii na hata nje ya Afrika amekiona na ataungana na sisi kuwapongeza kwa soka safi na la ushindani walilolionyesha kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Leo hii Ligi ya Tanzania imeingia midomoni mwa watu kwa sababu ya mafanikio ya klabu zetu, hii itaongeza ushawishi kwa wachezaji wa nje ya Tanzania kutamani kuja kucheza ligi ya hapa nchini hususani kwenye klabu kubwa za Simba, Yanga na Azam.

Uwezo na ushindani waliouonyesha Yanga kwenye michuano hii umemfanya Rais wa nchi yetu, Samia Suluhu kuwapa mwaliko wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa kupata nao chakula cha mchana kwa lengo la kuwapongeza.

Rais Samia ameona jitihada za klabu hii katika kulitangaza taifa kwenye mashindano ya kimataifa, mafanikio ya Yanga ni mafanikio ya nchi kwenye soka, sasa Afrika inafahamu uwezo wa klabu zetu kwenye mashindano ya kimataifa.

Hakuna ubishi Yanga wanastahili pongezi kwa kile walichokifanya msimu huu kwenye michuano ya kimataifa, kupata ushindi mbele ya wenyeji hasa klabu za Afrika Magharibi sio jambo dogo hata kidogo.

Miaka ya nyuma tulizoea kuona klabu zetu zikienda nje ya nchi zinafuata vipigo na pengine matokeo ya kudhalilisha, lakini kwa sasa mambo yamekuwa tofauti, klabu za Tanzania zinaweza zikapata matokeo ugenini.

Kile walichokifanya Yanga kinapaswa kuigwa na klabu zingine za Tanzania hususani zile zitakazopata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao.


Yanga na Simba tayari zimejihakikishia kucheza michuano ya kimataifa mwakani, lakini Azam na Singida Big Stars nazo zimeshatanguliza mguu mmoja kushiriki mashindano ya kimataifa, kile walichokifanya Yanga wanapaswa kukiiga.

Hakuna ubaya kuiga mafanikio ya mpinzani wako, Simba, Azam na Singida ziige kile ambacho Yanga wamekifanya msimu huu, zijiandae na zijipange kufanya vizuri, hakuna kinachoshindikana kwenye soka unapokuwa na nia na malengo.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Klabu Tanzania zikijipanga zitatwaa ubingwa Afrika

Na Adam Fungamwango

**NILICHOKISHUHUDIA** kwenye michuano ya kimataifa msimu huu ni kufanya vema kwa timu za Tanzania, Simba na Yanga huku kikubwa zaidi zikiwa hazina hofu tena zinapocheza ugenini kwenye nchi za Afrika Magharibi.

Juzi tumeshuhudia wachezaji wa Yanga wakipambana uwanja wa USMA Algers ya Algeria mbele ya mshabiki wake lukuki waliokuwa wakishangilia uwanja mzima, wakiwasha miale, fashifashi na vitatarizi vingine ambavyo vilikuwa vinatoa moshi kiasi kwamba waliokuwa wanatazama kwenye televisheni wakati mwingine hawaoni kitu.

Kwenye mchezo huo wa fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Yanga ilishinda bao 1-0, lakini ilishindwa kutwaa kombe hilo kwa kanuni ya bao la ugenini, ikichapwa mabao 2-1 awali nyumbani.

Kilichoonekana ni kwamba angalau sasa tumeanza kuona wachezaji wa timu za Kitanzania wakicheza bila kuhofia au kutolewa kwenye mchezo na mashabiki wa nchi zinazoitwa za kiarabu, wenye kila aina ya vurugu.

Zamani timu kutoka Tanzania ilikuwa ni aghalabu kucheza kwa utulivu zinapocheza mbele ya mashabiki wa aina ile, lakini inavyoonekana uwekezaji wa klabu zetu kwa kusajili wachezaji ambao wameshawahi kucheza michuano mikubwa mbele ya halaiki ya mashabiki 'vichaa wa soka' kama wale walioonekana nchini Algeria, imesaidia sana.

Timu zetu zilipokuwa zikienda kucheza na timu kama za Misri, Algeria, Tunisia, Morocco, kupigwa kuanzia mabao manne, matano mpaka sasa kutokana na kuchanganywa na aina ile ya mashabiki.

Yanga ilipambana kiume na hawakuruhusu mashabiki wa USMA kuwatoa mchezoni, lakini kwa bahati mbaya wakashindwa kutwaa kombe.

Nilishuhudia pia mechi ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Simba dhidi ya Wydad Athletic Club ya Casablanca, Morocco ambapo pamoja na kujazana na kushangilia kwa nguvu zote, lakini wachezaji wa timu ya Tanzania walikaa imara dhidi ya mabingwa watetezi kiasi kwa kwenda kutolewa kwenye hatua za matuta.

Simba iliikamata kisawasawa Wydad kiasi cha mashabiki waliokuwa wanashangilia kunyamaza na kuanza kuomba dua ili wapate ushindi.

Hii inaonyesha kuwa tayari timu za Tanzania zimeshaanza kuzoea kucheza na timu za Uarabuni, hivyo kinachofuata ni kwamba ubingwa wa Afrika na Kombe la Shirikisho upo njiani.

Nasema hivyo kwa sababu timu za Uarabuni ndizo kwa kiasi kikubwa zinachukua makombe hayo na zimekuwa zinaogopwa mno hasa zinapocheza nyumbani, lakini kitendo cha timu za Simba na Yanga kuanza kuziburuza zikiwa kwao, ni ishara tosha kuwa kuna kitu kiko njiani.

Na hata ukiangalia mechi zote hizo za Simba na Yanga ilikuwa kidogo zifanikiwe zikiwa ugenini, Yanga kutwaa ubingwa na Simba kutinga hatua ya nusu fainali.

Na hili ndilo lilikuwa linatumiwa sana na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kipindi hicho ikiwa timu ya kutisha. Ilikuwa ina uwezo wa kuzifunga timu za Kiarabu hata kwao, hivyo kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Afrika.

Ubingwa wa Afrika au Kombe la Shirikisho ni lazima uzifunge timu hizo kwao, na naona taratibu timu za Tanzania imeanza mageuzi hayo taratibu.

Kinachotakiwa sasa ni viongozi wa timu zinazoiwakilisha Tanzania, kuendelea kusajili wachezaji wazoefu, si kwenye michuano hiyo tu, bali wenye uwezo wa kucheza kwenye presha ya mashabiki wa timu za Kiarabu ambazo zimekuwa zikitunyanyasa miaka nenda rudi.

Hizi tunazoziona ni dalili njema kwa klabu za Tanzania, kama zimeanza kuwakimbiza Waarabu mbele ya mashabiki wao, kama uwekezaji wa wachezaji bora ukiongezwa, si miaka mingi tutatwaa Kombe la Shirikisho na Ligi ya Mabingwa Afrika.

## HABARI KITAIFA

# Tanzania na Kenya zakubaliana kuimarisha mipaka ya kimataifa

**Na Munir Shemweta,** ARUSHA

TANZANIA na Kenya zimetia saini hati ya makubaliano ya mpango kazi wa utekelezaji wa kuimarishaji mpaka wa kimataifa baina ya nchi hizo awamu ya tatu kutoka Namanga mkoani Arusha hadi Tarakea, Kilimanjaro wenye urefu wa Km 110.

Hatua hiyo inafuatia kikao cha Kamati ya Pamoja cha Wataalamu (JTC) kilichofanyika kwa siku tano jijini Arusha kuanzia Mei 29 hadi Juni 2 mwaka huu kwa lengo la kupokea taarifa ya ukaguzi wa kipande cha awamu ya tatu, kufanya ukaguzi katika eneo linaloimarishwa na kuandaa mpango kazi wa awamu zinazofuta.

Utiaji saini makubaliano ya mpango kazi baina ya pande hizo mbili ulifanyika mwishoni mwa wiki mkoani Arusha kati ya Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Hamdouny Mansoor na Juster Nkoroi, Ofisa Mtendaji Mkuu Ofisi ya Mipaka ya Kimataifa Kenya (KIBO) na kushuhudiwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Lucy Kabyemera.

Miongoni mwa makubaliano yaliyofikiwa ni kuendelea na uimarishaji mpaka awamu ya tatu kipande cha Km 110 (Namanga-Tarakea), kuwa na kikao cha Kamati ya Wataalamu (JTC) mwezi Septemba mwaka huu ili kupokea taarifa ya kazi ya uwandani na timu za wataalamu kukutana na kuandaa taarifa na rasimu ya mpaka ulioimarishwa.

Akizungumza wakati wa kufunga kikao hicho, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Lucy, alisifu kazi iliyofanywa na wataalamu wa pande hizo mbili hadi kufikia mwafaka wa kuendelea na kazi awamu ya tatu na kuahidi Serikali ya Tanzania iko bega kwa bega kuhakikisha kazi inafanikiwa.

"Nichukue fursa hii kuwahakikishia wataalamu wa pande zote kuwa serikali imejipanga kuhakikisha kazi hii inakamilika kama tulivyokubaliana," alisema Lucy.

Balozi Mdogo wa Kenya mwenye makazi yake jijini Arusha, Balozi Dennis Mburu, alisema makubaliano yaliyofikiwa yanaonyesha uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi hizo mbili na ni imani yake uhusiano huo utaendelea kudumu.

Katika siku ya pili ya kikao, Kamati ya Pamoja ya Wataalamu wa nchi hizo mbili ilitembelea eneo la mpaka wa kimataifa lililoko Mto Losoyai mkoani Kilimanjaro unaoungana na Ruvu kuingia Ziwa Jipe na kufuatiwa na mpaka wa nchi kavu hadi Pangani kwa lengo la kujiridhisha.

Wakiwa katika eneo hilo, wajumbe wa kamati hiyo wakioongozwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Mansoor na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Mipaka ya Kimataifa ya Kenya (KIBO) Juster Nkoroi, walijionea uhalisia wa mpaka na changamoto za eneo hilo.

Kikao cha siku tano kilichofikia makubaliano ya kuendelea na kazi ya uimarishaji mpaka wa kimataifa awamu ya tatu pia kimepokea taarifa ya awali ya ukamilishaji kazi zote za awamu ya kwanza na ya pili yenye jumla ya Km 348 ambazo tayari zimeimarishwa.

Kikao hicho pia kimeandaa mpango kazi kwa awamu zinazofuata za nne na tano kuanzia eneo la Tarakea mkoani Kilimanjaro hadi Jasini wilayani Mkinga mkoani Tanga, eneo lililopo ufukweni mwa Bahari ya Hindi linalokamilisha jumla ya kilomita 758 za nchi kavu za mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya.

## ACT yataka Sheria ya Madini imulikwe

**Na Julieth Mkireri,** GEITA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema serikali inapaswa kutazama upya Sheria ya Madini na sera zake ili madini ya kimkakati yaache athari chanya nchini hususani kwa maeneo husika.

Pia kimesema serikali inapaswa kusimamia kujengwa kwa miji ya madini karibu na maeneo ya uchimbaji ili kuongeza kilichokiita mzunguko wa shughuli za kiuchumi. Katika mkutano wa hadhara uliofanyika mjini Geita jana, Kiongozi wa Chama hicho, Zitto Kabwe alisema wachimbaji wadogo wanachangia zaidi ya asilimia 40 ya mapato yatokanayo na madini na kuajiri watu zaidi ya 218,353 lakini hali zao bado ni mbaya.

Zitto alisema hali za wachimbaji hao wadogo zimeendelea kuonekana mbaya kutokana na kufanya kazi katika mazingira hatarishi huku wakiwa hawana zana za kisasa za kufanyia kazi zao. Kiongozi huyo alisema maendeleo ya sekta ya madini yanatakiwa kwenda sambamba na maendeleo ya watu na maeneo yao kwa kuweka mikataba ya sheria na mgawanyo wa mirabaha.

Zitto pia alizungumzia suala la katiba mpya, akisema ACT-Wazalendo inataka kufikia mwishoni mwa mwaka huu iwe imepatikana.

Alisema kuna haja Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 ihuishwe kwa kuweka utaratibu mpya wa kukamilisha mchakato wa katiba. Pia iundwe timu ya wataalamu ili kuandika rasimu mpya ya katiba na kura ya maoni ya katiba mpya.

Chama hicho pia kimeelekezwa kutungwa kwa sheria mpya ya uchaguzi ili kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi na kutungwa Sheria mpya ya Vyama vya Siasa.

"Tutoke kwenye maneno twende kwenye vitendo. Tutoke kususasusa twende kwenye mazungumzo ili kupata katiba mpya na Tume huru ya Uchaguzi," alisema Zitto.

Naibu Waziri Kivuli wa Elimu, Bahati Chirwa, alisema lipo tatizo la kukithiri kwa michango katika sekta ya elimu ambalo linasababisha baadhi ya watoto kushindwa kwenda shuleni.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**MWALIKO WA MAFUNZO YA MATUMIZI YA MIFUMO YA KIELEKTRONIKI YA USIMAMIZI WA KODI YA ZUIO ILIYOBORESHWA (UPGRADED WITHHOLDING TAX MANAGEMENT SYSTEMS)**

**Dar es Salaam, 2 Juni, 2023:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inapenda kuwajulisha walipakodi walio katika kundi la taasisi za umma nchini kuwa itafanya mafunzo maalum ya matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa kodi ya zuio (Withholding Tax) kufuatia maboresho yaliyofanyika hivi karibuni. Semina hii itafanyika siku ya J**umanne tarehe 6 Juni 2023** mkoani **Dodoma** katika Ukumbi wa **African Dream Hotel** kuanzia **Saa 3:00** asubuhi na itaendeshwa na TRA Makao Makuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango.

Walipakodi walio katika kundi hili wanahimizwa kushiriki mafunzo haya ili kujijengea uwezo wa kuitumia mifumo hiyo kwa ufasaha na kuziwezesha taasisi kutimiza matakwa ya sheria na taratibu zinazosimamia utozaji wa kodi hiyo.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

Tovuti : www.tra.go.tz
Piga simu bure : 0800-110016 au 0800-750 075 au 0800-780 078
WhatsApp : 0744 23 33 33
Barua Pepe : huduma@tra.go.tz

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

RIPOTI MAALUM - SIKU YA MAZINGIRA

# Dampo Pugu Kinyamwezi kulivyosheheni uchafu wa ofisi, watendaji hadi mlo wao

**Na Christina Mwakangale**

DAR es Salaam iko hatarini. Dampo pekee linalotegemewa na wakazi wilaya tano limejaa na hakuna mkakati wowote wa watendaji kulifanya liwe la kisasa.

Kukua kwa mkoa huo na idadi kubwa ya wakazi inayofika milioni 5.4 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, kunatajwa kuongeza ugumu kuanzia udhibiti hadi uondoaji wa taka katika makazi, masoko na ofisi.

Uchunguzi wa Nipashe uliofanyika kwa miezi miwili, umebaini dampo hilo pekee linaloitwa Pugu Kinyamwezi halifai tena kwa shughuli za uhifadhi endelevu wa taka.

Tovuti rasmi ya Jiji la Dar es Salaam ina taarifa za kuwapo makadirio ya kuzalishwa taka takribani tani 4,600 kwa siku jijini, huku asilimia 45 hadi 50 pekee ndizo zinazopelekwa dampo kutoka wilaya za Kigamboni, Ilala, Ubungo, Temeke na Kindondoni, sehemu kubwa ni kutoka wilayani Ilala.

Nipashe imebaini vikwazo vyake vinafanana na miji mingine, hata kutoa funzo la pamoja katika ukuaji wa jiji.

Dampo la Pugu Kinyamwezi lipo wilayani Ilala, umbali wa kilomita 30 kutoka katikati ya mji. Lina ukubwa wa hekta za mraba 65 sawa na ekari 162, mabadiliko yanayochukua nafasi kwa miaka 16 sasa.

Hali ilivyo sasa, dampo limejaa, Nipashe ikiwa na ushuhuda unaoendana na malalamiko wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Amos Makalla, wiki chache kabla ya kuhamishwa kituo cha kazi kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

Mwonekano wa dampo kwa sasa ni mithili ya kimo cha ghorofa tatu, wabebataka wa eneo hilo wakisema kujaa kwa dampo, kunawanyima fursa za kipato cha kila siku. Majirani wa mahali hapo, wanalalamikia harufu, kutowekwa ukuta kunakosababisha taka nyepesi kupeperuka hadi katika makazi yao na kwingineko.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Amani Mafuru, anasema Halmashauri ya Jiji la Ilala, kunakopatikana dampo hilo linalopokea taka za wilaya zote za Dar es Salaam, ndilo inayozalisha taka zaidi. Inakadiriwa kuzalisha tani 1,100 kwa siku na uwezo wa kuondosha taka hizo kwenda Dampo la Pugu Kinyamwezi ni tani 620 pekee kila siku, sawa na asilimia 56.

**USHUHUDA WA NIPASHE**

Kinacholalamikiwa Pugu Kinyamwezi, kinaisukuma Nipashe kuzuru kikazi kwenye dampo kujionea hali halisi.

Ilikuwa saa 2:30 asubuhi ya tarehe 24 mwezi uliopita, mwandishi alipowasili Pugu Kinyamwezi, ambako ni wastani wa kilomita 29 kutoka Soko la Kimataifa la Kariakoo.

Unaposhuka liliko dampo hilo maarufu, ushuhuda wa kwanza ni mwonekano wa 'mlima' utokanao na lundo la uchafu, wastani wa kimo cha ghorofa tatu.

Kadri mtu anapokaribia kuelekea barabara iliyojengwa kwa zege mwendo wa hatua 380 au mita kwa wajuzi wa hesabu, anakifikia kifusi hicho. Hapo mara moja anabaini uhalisia wa kilichoko, ni kifusi cha taka. Baada ya salamu za Nipashe kwa wenyeji ambazo zikapokewa kwa ushirikiano wa karibu na mmoja wao aliyeko kazini damponi, akiwa sehemu ya kundi la watu saba; mwanamama mmoja, waliobaki ni kinababa vijana, wenye umri wa kati na watu wazima.



Sehemu ya fukwe ya Aga Khan jijini Dar es Salaam ikiwa imetapakaa uchafu na kuweka mwonekano mbaya kwenye eneo hilo.

Mandhari yao yameundwa na turubai chakavu linalokaribia kudondoka, lakini linawasitiri dhidi ya juakali lililokuwa linawaka wakati huo.

Anayemsogelea ni mwandishi wa habari, kijana asiyejificha ucheshi wake. Anatoa ushirikiano wa karibu kwa mgeni huyo, ambaye yuko dhahiri kuanzia kwa mavazi, si anatofautiana sana na wenyeji aliowakuta, wakiwa katika mavazi kuukuu, chakavu na yasiyo safi.

Hapo Nipashe inajifunza kupitia haiba na matendo yao, wapo hapo kwa ajili ya kupekua taka, kusaka wanavyovitaka, ikiwamo bidhaa za plastiki. Ndiyo riziki yao.

Hapo mwenyeji huyo anayejitambulisha kwa jina la Omary, anaanika uhalisia akiwa na ufafanuzi: "Kwa mazingira ya hapa muda wote ni tope, huwezi kupita hasa msimu huu wa mvua. Ngoja nikuagizie buti! Ila buti ambayo ni mpya unakodishwa kwa Sh. 500 na iliyotumika Sh. 300." Mwandishi anaridhia ushauri kwa kuvaa.

Safari inaendelea, kadri unavyolikaribia dampo, ndivyo harufu mbaya, nzi, kunguru na paka wanavyoshuhudiwa kwa wingi. Ni taka za kila aina, nepi za watoto za kisasa (pampasi) zilizotumika, baadhi zikiwa na vinyesi, mifuko ya plastiki iliyotumika kubeba bidhaa kama vile sabuni, pia mabaki ya vyakula.

Kadri unavyopigwa hatua, ndivyo unavyoifikia ardhi yenye unyevu, ikibonyea mithili ya godoro, hadi kufika katika kibanda kilichojengwa kwa zege na kuzungushiwa wigo wa chuma. Hapo Omary anadokeza ndipo penye ofisi rasmi ya dampo.

Haiba ya mgeni mwandishi ilionekana kuwapa butwaa wenyeji ofisini, waliokuwa watatu. Pembeni mwa ofisi kukiwapo madumu takribani 10 ya lita 20 yenye michirizi ya mafuta kwa mwonekano, ama ni petroli au dizeli.

Utambulisho unaendelea, mwenyeji akikiri ni kiongozi wa dampo, huku akijihami hayuko tayari kuzungumza, ila akatoa rukhsa Nipashe iendelee kukagua.

Pembeni mwa ofisi, nako kulikuwapo gari kubwa mithili ya injini, wenyewe wanaliita buldoza. Limenasa katika tope la uchafu hadi matairi kutoonekana.

Mara moja, bosi huyo anamtamkia kijana mmoja aliyevaa vazi la kiufundi 'overall' kwamba 'wee chukua hilo dumu, peleka pale' (kati ya madumu 10 yaliyokuwapo pembeni)..."

Kijana huyo akatekeleza kwa kuondoka nalo. Nipashe inabaini ni biashara isiyo rasmi ya mafuta. Magari yamezama katika tope, lakini halmashauri inapeleka mafuta ili kuhudumia dampo.

Mwandishi anatumia rukhsa aliyopewa, kuhamia liliko buldoza lililonasa. Hapo napo wenyeji wanasogea. Mmoja wa vijana akatokea katikati ya mlima wa dampo, akatoa ufafanuzi:

"Hili 'buldoza' ndio mkwamo! Limeharibika muda mrefu na taka haziwezi kusambazwa. Taka zimeweka mlima, huwezi kuzifukua, ili tupate riziki zetu."

Kulia mwa dampo, kulikuwa na mtu mwenye umri wa makamo akiwa na jembe lenye 'meno' marefu mithili ya reli, pia mfuko mkubwa wa plastiki kama inayohifadhi taka hospitalini, ndani yake amejaza mifuko mingine ya plastiki.

Vilevile, mahali hapo kulishuhudiwa vijana watano, wakinywa chai na mihogo pasipo shaka yoyote, wakipewa huduma na mama aliyevalia dera, wanywaji chai hao wameketi juu ya 'chesesi' ya lori lililoharibika.

Mwenyeji mwingine anayejitambulisha kwa jina moja la Side, naye anajiunga na Nipashe, akisimulia uzoefu wake mahali hapo kwa kauli "...waokotataka hapa dampo mara nyingi wengi wao ni walevi, sijui kwanini! Pengine ni kutokana na mazingira ya kazi hii!

"Mimi ninachookota hapa ni mifuko ya sabuni, hata vifaa, kwa sababu kuna wakati unabahatika kuokota kitu cha thamani. Si unajua matajiri wengi hutupa vitu vya thamani! Kwa siku ninagombea kuipata Sh. 1,000 au 500."

Baadaye mwandishi anahamisha udadisi huo kwa mtaalamu wa saikolojia, William Nkuhi, kupata ufafanuzi. Mtaalamu huyo anatoa tafsiri ya mlo na makazi kufanyika katika mazingira hayo machafu, akitamka:

"Wanaangukia katika ugonjwa sugu wa kisaikolojia unaoitwa 'Substance and Drugs Abuse or Disorder'.

"Ni kweli, pia kuna watu hushinda katika majalala miaka na miaka na hawa tunawaweka katika kundi la watu wenye magonjwa ya akili yanayosababishwa na mfumo wa maisha."

**Fuatilia kesho, kazi na maisha ya kila siku jalalani Pugu Kinyamwezi.**



# KCMC yapokea wagonjwa afya ya akili 300 kwa mwezi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

DAKTARI bingwa wa afya na magonjwa ya akili wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Dk. Editruda Gamassa, amesema hivi sasa wanapokea wagonjwa wa nje wenye matatizo ya afya ya akili, zaidi ya 300 kwa mwezi mmoja.

Magonjwa ya afya ya akili ambayo ni tishio nchini ni Kihoro (Anxiety), Sonona (Depression), PTSD-Trauma (Post Traumatic Stress Disorder), Baipola (BPD), Skizofrenia na Uraibu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha kushirikisha wadau matokeo ya mradi wa afya ya akili, uliotekelezwa kwa miezi sita na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization (KWIECO) katika Kata za Uru Kusini, Uru Mashariki na Kibosho Kindi katika Wilaya ya Moshi, Dk. Gamassa alisema kutokana na ongezeko hilo la wagonjwa wa afya ya akili, kwa sasa wanalazimika kutoa huduma ya kliniki mara mbili kwa wiki. Kwa mujibu wa Dk. Gamassa, hospitali ambazo zinatoa huduma ya kliniki ya afya ya akili kwa wagonjwa wa nje katika Mkoa wa Kilimanjaro ni Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi) na KCMC.

"KCMC kwa mwezi, huwa tunawaona na kuwahudumia wagonjwa hadi 300 kama wagonjwa wa nje, kwa sababu kliniki tunafanya mara mbili kwa wiki na tunawaona wagonjwa wa aina mbalimbali, wenye matatizo ya afya ya akili kuanzia magonjwa kama ya sonona, wasiwasi au hofu iliyopitiliza, skizofenia, baipola na pia watu wenye matatizo ya uraibu, hasa utumiaji wa vilevi kama pombe, bangi na wachache wanaotumia dawa za kulevya kama heroine.

"Kwa wa upande wa matibabu, sana sana tunatoa huduma kwa wagonjwa wa nje, yaani matibabu kwa aina ya dawa kulingana na ugonjwa alionao na tunatoa huduma za kisaikolojia, tiba za saikotherapia (tiba ya maongezi); na pia tunatoa tiba ya vitendo," alisema Dk. Gamassa.

Akitoa maelezo kuhusu mradi wa afya ya akili, unaojumuishwa na ukatili wa kijinsia, Mratibu wa mradi huo unaoendeshwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Shirika la CROSSROAD International, Immaculate Mworia, alisema baada ya kufanyika mradi wa majaribio katika Kata tatu za Uru Kusini, Uru Mashariki na Kibosho Kindi, Wilaya ya Moshi, umeonyesha uhitaji mkubwa kutokana na kuwapo kwa wagonjwa wengi wa afya ya akili.

"Mradi huu, uliolenga kutoa elimu ya afya ya akili, unaoshirikishwa na ukatili wa kijinsia kwa jamii na kwenye jamii yenye malengo ya mradi ni kufikia idadi ya wanajamii 300, wazazi wenye wanafunzi katika shule tatu wapatao 300 na kuwafikia wanafunzi 300.

"Aidha, mradi huu ambao ulianza rasmi Desemba 19, 2022 ni mradi mfupi wa majaribio yaani Pilot Project, ambao umefanyika ndani ya miezi sita ambapo mwezi Mei 2023," umefikia ukomo wake.

Zaidi aliongeza, "baada ya kufanya tathmini na Moshi DC (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi), tulielekezwa maeneo yenye watu wenye changamoto za akili. Tulipewa maeneo mengi, lakini kutokana na ukweli kwamba ni mradi wa majaribio, tuliibuka na kata tatu na tunashukuru tumewafikia wanajamii kwanza na kuwaelimisha kuhusu ukatili wa kijinsia, unaweza kuwa kisababishi cha ugonjwa wa akili."

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastory Msigala, ambaye aliwakilishwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Lucas Msele, alisema katika mradi huo jamii na hasa wanafunzi katika kata zilizolengwa na mradi, wamepata kitu fulani hata kama hawatoenda kukisema kwenye jamii nje, lakini kwenye familia anayotoka atakuwa mlinzi na mfuatiliaji wa mambo hasa yanayoashiria dalili za kuwapo mtu mwenye tatizo la afya ya akili.

Katika kikao hicho, Mwalimu Cecilia Mwolere kutoka Shule ya Sekondari ya Mnini, alisema mradi huo umewasaidia kwa kiasi kikubwa kupata uelewa, ambao watautumia kuiamsha jamii ya Uru Mashariki, ambako kuna waathirika wengi sana.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Uru Kusini, Prisca Ramadhan, alisema mradi huo baada ya kufika kwenye jamii yao na kutoa elimu juu ya visababishi vya magonjwa ya afya ya akili, umewasaidia kupunguza idadi ya vijana wanaotumia vilevi aina ya pombe kupitiliza.

# DC akabidhi madawati 50 Shule ya Msingi Endiamtu

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, amekabidhi madawati 50 kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Endiamtu, inayokabiliwa na upungufu wa madawati.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya madawati hayo, Dk. Serera, alisema amekabidhi madawati 50 baada ya kukuta shule hiyo ina upungufu wa madawati hivyo aliwatafuta wadau mbalimbali wa maendeleo na walichukua jukumu la kuwasaidia wanafunzi hao.

"Madawati haya yatapunguza tatizo kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Endiamtu. Nawaomba wenyeviti wa vitongoji wa kata hii, kupitia mikutano ya hadhara ya wananchi, mwangalie namna ya kujitoa na kuchangia madawati ili kumaliza tatizo tulilonalo sasa," alisema.

Awali Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Evetha Kyara, alimshukuru Mkuu huyo wa wilaya kwa kuwapatia madawati kwa kuwa wamefikia asilimia 71 ya mafanikio na kiwango kilichobaki ni asilimia 21.

Kyara alisema madawati hayo yaliyotolewa na kiongozi huyo, yatatumiwa na wanafunzi 150 na itasaidia kupunguza tatizo hilo, kwa kuwa baadhi ya madarasa, dawati moja linakaliwa na wanafunzi watano.

Shule hiyo, ina wanafunzi 981, ambao wavulana ni 505 na wasichana 476, huku ikiwa na mahitaji ya madawati 350, yaliyoko sasa ni 258 na pungufu ni 102.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alimshukuru Dk. Serera, kwa kufanikisha upatikanaji wa madawati hayo.


TEMBO NICKEL

TANGAZO LA UTEUZI



**Benedict Busunzu**
**Mtendaji Mkuu (CEO) Tembo Nickel**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Tembo Nickel, ninayo furaha kutangaza uteuzi wa Bw. Benedict Busunzu kama Mtendaji Mkuu (CEO) wa kampuni ya Tembo Nickel, kampuni yenye ubia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye lengo la kuleta umahiri katika uchimbaji madini na manufaa kupitia mgawanyo sawa wa faida za kiuchumi. Benedict anaanza kutekeleza majukumu mara moja. Katika utekelezaji wa majukumu haya, Benedict anawajibika moja kwa moja kwa Bodi ya Wakurugenzi.

Benedict ameitumikia kampuni ya Tembo Nickel kama Mkurugenzi Mkazi tangu alipojiunga na kampuni mnamo tarehe 1 Agosti 2021.

Benedict ana miaka kumi na nane ya uzoefu mpana katika kusimamia operesheni za uchimbaji madini, ametumikia miaka kumi na mbili kati ya hiyo katika ngazi za uandamizi kwenye tasnia ya uziduaji. Benedict ana uzoefu wa kazi na elimu katika nchi za Tanzania, Afrika Kusini, Uingereza na Australia.

Kutokana na uzoefu wa awali katika majukumu ya kibiashara kama Meneja Mkuu pamoja na Meneja wa Biashara, Benedict ana utaalam mahususi katika kuongoza timu za mataifa mbalimbali na zenye tamaduni tofauti, ana maono na uwezo wa kupanga mikakati yenye kukuza thamani ya miradi, uwezo wa kujenga mahusiano mazuri na bodi, wawekezaji pamoja na ngazi za juu za serikali na mahusiano ya jamii.


Kabla ya kujiunga na Tembo Nickel, Benedict alikuwa Meneja Mkuu wa kampuni ya Twiga Minerals (inayoundwa kwa ubia kati ya kampuni ya Barrick Gold Corporation na Serikali ya Tanzania), ambapo alisimamia uendeshaji wa operesheni katika migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi.

Ni furaha yetu kumkaribisha Benedict katika majukumu yake mapya hapa Tembo Nickel. Bodi inatarajia kuona mafanikio na maendeleo zaidi ya Mradi.

Bw. Keith Liddell
Mwenyekiti wa Bodi
**Tembo Nickel**
**www.tembonickel.com**

Akizungumzia uteuzi wake Benedict amesema, "Ni heshima kubwa kuteuliwa kuwa kati ya Timu ya Uongozi ya Tembo Nickel, kampuni tunayoamini itazalisha nikeli ya kwanza ya kiwango cha betri kutoka katika mgodi mpaka kufikia nikeli iliyosafishwa na kuhakikisha uwepo wa manufaa kamili ndani ya nchi. Ninatizamia kuendeleza safari ya kujenga kampuni hii inayokua pamoja na kufanya kazi na timu mahiri ambayo kati yao wamepandishwa vyeo kuunda Kamati Tendaji ya Uongozi. Kwa pamoja tutafanikiwa kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.

Hapa Tembo Nickel, tumejidhatiti kutimiza vyema uzingatiaji wa kanuni za Usalama wa Mazingira, Jamii pamoja na Uongozi Bora (ESG): Usalama, Ushirikiano na wenyeji, Kupunguza Madhara katika Mazingira, Kuendesha Kazi kwa Uwazi, Kuwajibika katika Mnyororo mzima wa kutoa huduma zetu na Maendeleo ya Jamii.





## Wagonjwa 1,000 hawapati matibabu ya fistula

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KILA mwaka wanawake 2,500 hadi 3,000 wanapata ugonjwa wa fistula nchini huku kati yao 1,500 hadi 2,000 ndiyo wanaopatiwa matibabu ya ugonjwa huo huku zaidi ya wagonjwa 1,000 wakikosa matibabu na kuufanya kuendelea kuwa tishio.

Takwimu hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Americares Foundation Tanzania, Nguke Mwakatundu, wakati wa kukabidhi vifaa vya upasuaji wa fistula ya uzazi katika Hospitali ya Rufani Kanda Bugando vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 234.2 na kusema kuwa tatizo hilo bado ni kubwa na linahitaji msaada kulikabili.

"Hii ndiyo sababu tumeamua kununua vifaa maalumu kwa ajili ya upasuaji wa fistula ya uzazi katika Hospitali hii ya Bugando, lengo likiwa ni kuhakikisha hospitali inaendelea kutoa huduma hii kwa utaalamu na ufanisi zaidi na tumekuwa tukifanya hivi kila mara lengo kuu ni kurejesha tabasamu kwa wanawake wenye tatizo hili," alisema.

Aidha, alisema ili kuhakikisha tatizo la fistula linatokomezwa kufikia 2030 shirika hilo litaendeleza ushirikiano wa karibu zaidi huku akiiomba serikali kuziwezesha hospitali za mikoa kutoa huduma hiyo lengo likiwa ni kuhakikisha wanawake wanaosumbuliwa na ugonjwa huo kupata huduma kwa karibu na sio kuifuata umbali mrefu.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani Kanda Bugando, Dk. Fabian Masaga, alisema jamii bado haina uelewa wa fistula wanaendeleza mapambano ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwaajili ya kudhibiti ugonjwa huo na uelimishwaji wa wauguzi na wakunga kuhakikisha wanatoa huduma bora ya uzazi kwa wanawake.

Aidha, alisema kila mwaka wagonjwa 300 hadi 400 wanapokewa katika hospitali hiyo na kuonesha kuwa ugonjwa huo bado ni tatizo kubwa kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa huku mikoa inayoongoza ikiwa ni Geita na Shinyanga.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema serikali itaendelea kuwa bega kwa bega kushirikiana na mashirika binafsi likiwamo Americare ikiwa ni pamoja na kuwaondolea ushuru wa vifaa wanavyotoa bure kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huo lengo likiwa kufanya kazi katika mazingira rafiki nchini.

Aliwataka wahudumu wa afya kuendelea kutoa huduma bora kwa wagonjwa ili kuhakikisha wanarejesha tabasamu ambayo wagonjwa wao wameikosa kwa muda mrefu na pengine kutengwa na jamii.

Baadhi ya waathirika wa fistula kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa akiwamo Pendo Bonephas, mkazi wa Mara alisema alipata ugonjwa huo kutokana na kujifungua kwa njia ya upasuaji na kukataliwa na mume wake ambaye aliitelekeza familia.

Alisema, huduma ya matibabu wanaipokea bure na kutoa shukrani kwa wadau wanaofadhili huduma hiyo ikiwa ni pamoja na chakula, zawadi mbalimbali zinazowapa motisha na kuendelea kujiona sehemu ya jamii na kuheshimika.

# Mradi wa maji vijiji 15 wafikia asilimia 75

**Na Restuta Damian,** KYERWA

MRADI wa miundombinu ya mabwawa na matangi ya maji unaotarajiwa kutoa huduma kwa vijiji 15 katika kata za Runyinya, Kimuli na Nyamiaga, wilayani Kyerwa mkoani Kagera wenye thamani ya Sh. bilioni 8.13 umefikia asilimia 75 huku utekelezaji ukitarajiwa kukamilika Septemba 2023.

Meneja wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilaya, Mhandisi Shukrani Tungaraza wakati wajumbe wa Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kyerwa, wametembelea mradi huo unaotarajiwa kuondoa kero ya matumizi ya maji yasiyo safi na salama kutoka katika mabwawa. Alisema, yapo mahitaji makubwa ya usambazaji wa huduma ya maji kwa wananchi na kuwafikisha katika maeneo ya makazi kwa kutekeleza malengo ya wizara na serikali kumtua mama ndoo kichwani.

"Hii miradi ikikamilika itaunganishwa pia katika taasisi, ofisi za umma na wananchi kwa maana ya gati na wale wa majumbani ndio watakaonufaika na miradi inajengwa ndani ya wilaya," alisema.

Kadhalika, alisema shughuli za ujenzi wa miundombinu inaendelea katika maeneo mbalimbli ya vitongoji, vijiji, kata ili kuwa na maji kwa wananchi na kufikia mwaka 2025 kuwe na asilimia 85 hadi 90 iliyokusudiwa. Katibu wa CCM Wilaya ya Kyerwa, Fransis Kambona alisema, utekelezaji wa mradi huo ni mpango wa serikali wa kuhudumia jamii kupitia ilani ya chama, yenye kutaka miradi itekelezwe kwa manufaa ya wananchi na kuondoa matatizo kwenye jamii.

Diwani wa Kata ya Kimuli, Jonas Vedasto alisema, ukamilishwaji wa miradi hiyo utasaidia wananchi kupunguzia tatizo la matumizi ya maji yasiyo safi na salama kutoka katika mabwawa.

Alisema, Kata ya Kimuli ina vijiji vitatu na hakuna eneo ambalo wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama kwa kipindi kirefu.

"Licha ya miundombinu inayojengwa haitafikia asilimia zote katika kutoa maji kwa wananchi, lakini mategemeo ni asilimia 50 yawepo majisafi na salama na kuondoa tatizo la malumbano ya kifamilia," alisema Vedasto.



Ofisa Elimu Kata ya Ibinzamata, Manispaa ya Shinyanga, Mackrine Shija (kulia), akikabidhi vifaa vya shule kwa niaba ya Shirika la Sense International juzi kwa watoto wenye ulemavu katika kituo cha Buhangija walionusurika kifo baada ya bweni lao kuteketea moto na kupoteza wenzao watatu Novemba mwaka jana, (kushoto) ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija, Futama Jilala. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waganga tiba asili wapanda miti kulinda mitishamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA pamoja na waganga wa tiba asili katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamelazimika kupanda miti katika maeneo yao ya biashara kwa lengo la kuokoa dawa zao dhidi ya jua kali pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Imeelezwa kuwa dawa hizo zinazopatikana katika maeneo mbalimbali ya misitu huisha muda wake na kuacha kufanyakazi kwa ufanisi inapopigwa jua kali na pengine kukauka hali iliyowafanya wafanyabiashara hao wakiwamo watengenezea majeneza kuanza hatua za upandaji miti ili kuziokoa dawa hizo.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa tiba asili wilayani hamo, Kaliyaya Bashite, akizungumza wakati wa upandaji miti hiyo alisema, dawa za asili sio salama kiafya endapo zitakaa kwenye jua muda mrefu hali inawafanya kupoteza wateja wanaofika kutibiwa na kushindwa kupona maradhi yao, ndiyo maana imewafanya kupanda miti katika eneo lao la biashara ili kuepuka uharibifu wa dawa na majeneza.

Aidha, Bashite alisema, wamepanda miti hiyo kwa ajili ya kuhakikisha mazingira ya eneo hilo yanakuwa safi na kupata kivuli wakati wote wanapokuwa wakifanya biashara hiyo kwa kuwa eneo lao lipo kihalali kwa mujibu sheria kwa kuuza dawa asili na majeneza.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Masalu Kamuli alisema, eneo hilo halina kivuli na lipo jirani na geti la kuingilia Hospitali ya Manispaa ya Kahama na hata wanapopanga kufanya vikao vyao vinashindikana kufanyika kutokana na hali ya jua na moja ya sababu inayowafanya kupanda miti hiyo.

Alisema tayari wamepanda miti 22 ikiwa ni hatua endelevu ambako pia utakuwa msaada wa vivuli katika eneo hilo la biashara na kulinda mazingira dhidi ya ukame.

Nipashe
Spotika



MASTRAIKA AMBAO POCHETTINO ANATAKIWA KUWASAJILI CHELSEA 12 - 13




# MAKOCHA WA4 WALIOSHINDA KOMBE LA FA MARA NYINGI

**LONDON, England**

MWAKA 1990, Mark Robins alifunga bao katika ushindi wa raundi ya tatu wa Kombe la FA ambao hatimaye uliokoa kazi ya kocha wa Manchester United, Alex Ferguson ambaye wakati huo alikuwa amekalia kuti kavu.

Mashetani Wekundu walisonga mbele na hatimaye kulinyakua taji hilo likiwa la kwanza kwa Ferguson pale Old Trafford - na mengine yote yaliyofuata sasa imebaki kuwa historia.

Hakuna kocha yeyote ambaye ameweza kuwa katika kiwango cha juu kwenye uongozi wa klabu ya mpira wa miguu nchini England na akaaminika bila wasifu wake kuwa na Kombe la FA.

Na Jumamosi klabu za jiji moja la Manchester, Man City na Man United zilikutana kwenye fainali ya FA na kilichotokea kinajulikana.

Makala haya inawaangalia makocha wanne waliowahi kutwaa mara nyingi zaidi kombe la FA katika historia ya mashindano hayo.

**4. John Nicholson (Mara Nne)**

John Nicholson alikuwa Katibu Mkuu wa klabu ya Sheffield United kwa zaidi ya miaka 30 mwanzoni mwa karne ya 20. Katika kipindi hicho klabu haikuwa na kocha, hivyo Nicholson alichukua majukumu hayo pia.

Mtu huyo mashuhuri aliongoza kipindi cha mafanikio zaidi katika historia ya Klabu ya Sheffield maarufu zaidi kama Blades, akishinda Kombe la FA mnamo mwaka 1899, 1902, 1915 na 1925.

Pia alifika fainali mwaka 1901 na kushinda Ligi ya Daraja la Kwanza miaka mitatu baadaye, Nicholson bila shaka ni mmoja wa makocha bora zaidi katika historia ya awali ya soka licha ya kutoshikilia rasmi nafasi hiyo.

**3. Alex Ferguson (Mara Tano)**

Raia huyo wa Scotland alishinda mataji 38 makubwa katika miaka 27 ya utawala wake pale Old Trafford ambayo huenda yasifikiwe na kocha mwingine hivi karibuni.

Ferguson anaweza kujivunia ushindi mara tano wa Kombe la FA kwenda sambamba na mataji yake 13 ya Ligi Kuu ya England, EPL.

Mashetani Wekundu wamekuwa kwenye kiwango kisichovutia tangu Ferguson kuondoka, lakini walifanikiwa kushinda taji hilo mwaka 2016 chini ya kocha Louis van Gaal - kombe pekee la Mholanzi huyo katika kipindi chake cha utawala katika klabu hiyo.

**2. George Ramsay (Mara Sita)**

George Ramsay alikuwa Katibu Mkuu na kocha wa Aston Villa katika kipindi cha mafanikio zaidi cha historia yao mwishoni mwa karne ya 19.

Akiwa mchezaji, alijiimarisha haraka kama nahodha wa klabu hiyo na kuanza kufanya mapinduzi makubwa akichukulia ujuzi alioupata katika nchi yake ya Scotland.

Baada ya uchezaji wake kukatishwa haraka na jeraha, alihamia kwenye ukocha mnamo mwaka 1885 ambapo alifika fainali nane za Kombe la FA, akishinda sita, kati ya mwaka 1887 na 1924.

Villa pia walitawazwa mabingwa wa England mara sita chini ya Ramsay, ambaye anaaminika kuwa kocha wa kwanza katika soka la dunia kulipwa kwa kazi yake yenye thamani ya kila senti.

**1. Arsene Wenger (Mara Saba)**


Arsene Wenger ndiye kocha mwenye mafanikio zaidi katika michuano hii, akiiongoza Arsenal kushinda mara saba katika Kombe la FA wakati akiwa katika klabu hiyo.

Mfaransa huyo alikuwa mwanzilishi wa staili mpya ya ucheza wa soka nje ya ile iliyozoeleka ya Kiingereza na jina lake litahusishwa milele na kombe hilo.

Alishinda Kombe lake la kwanza la FA mnamo mwaka 1998 na la mwisho mnamo mwaka 2017 - mwaka mmoja kabla ya kumaliza kazi yake nzuri na Washikabunduki hao wa London.

## ISIKUPITE

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, ameiambia bodi ya klabu hiyo kuwa anataka kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspurs Muingereza Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, Ancelotti amesema Kane ni mshambuliaji mzuri aliyekamilika na ambaye anaweza akatoa mchango mkubwa ndani ya klabu hiyo hivyo bodi ya klabu hiyo ifanikishe mchakato wa kumsajili nyota huyo.



# MASTRAIKA AMBAO POCHETTINO ANATAKIWA KUWASAJILI CHELSEA



Pochettino

**LONDON, England**

UHITAJI kuwa Kocha Mauricio Pochettino ili kutambua ni kiasi gani Chelsea inahitaji mshambuliaji mpya.

The Blues wamekuwa 'wakiimarisha' safu ya ushambuliaji kwa miaka mitano iliyopita na bado wakajikuta kuwa na idadi mbaya zaidi ya wafungaji kwenye Ligi Kuu ya England.

Kwa kuwa Pochettino amewekwa rasmi kwenye kilingi cha kuinoa klabu hiyo ya pale Stamford Bridge ni zamu yake sasa raia huyo wa Argentina kujaribu kutafuta suluhu.

Pochettino alitangazwa kuwa kocha wa Chelsea wiki iliyopita akichukua nafasi ya Frank Lampard ambaye alirudi katika klabu hiyo kwa mara ya pili baada ya kutimuliwa mara ya kwanza.

Lampard alirudi kwa mara ya pili kama kocha wa muda hadi mwisho wa msimu akichukua mikoba ya Graham Potter aliyetimuliwa Aprili 2, mwaka huu ambaye alirithi mikoba ya Thomas Tuchel.

Pochettino mwenye umri wa miaka 51 ambaye alikuwa kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur na baadaye Paris Saint-Germain kabla ya kutimuliwa, amepewa mkataba wa miaka miwili kuinoa klabu hiyo na ataanza rasmi kazi Julai Mosi.

Akiwa amechukua mikoba hiyo, Pochettino ana kazi moja tu ya kurudisha siku za furaha za Chelsea na hapa tunawaangalia washambuliaji watano ambapo anapaswa kuwasajili mmoja wao kipindi hiki cha majira ya joto.

**#1. Victor Osimhen**

Akiwa mmoja wa wafungaji bora wa Ulaya msimu huu, mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen ni mmoja wa wachezaji wanaoweza kuisaidia Chelsea kwenye upachikaji wa mabao.

Akimtaja Didier Drogba kama ndio aliyemvutia zaidi, Osimhen mwenye umri wa miaka 24 amekuwa na hasira mwaka huu, akiongoza orodha ya wafungaji kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na kusaidia kuigeuza Napoli kuwa moja ya timu zinazotisha Ulaya.

Suala kuu hapa ni bei ya Osimhen. Napoli walikubali kulipa hadi euro milioni 80 walipomsajili kutoka Lille mnamo mwaka 2020 na imani ni kwamba anaweza kugharimu mara mbili zaidi ya kiasi hicho wakati huu.

**#2. Ivan Toney**

Ikiwa unataka mshambuliaji mwenye uzoefu wa Ligi Kuu ya England, Ivan Toney ndiye chaguo linalowezekana zaidi. Naam, hiyo ilikuwa hadi marufuku yake ya kutocheza soka kwa kipindi cha miezi nane kwa makosa ya kucheza kamari.

Huku msimu wake ukiwa umekamilika, Toney anamaliza kampeni akiwa na mabao 20 ya ligi akiwa na Brentford. Je, mara ya mwisho Chelsea ilikuwa na mchezaji wa kufikisha idadi hiyo ya mabao? Ndio, Diego Costa, miaka sita iliyopita.

Marufuku hiyo ni wazi inachanganya mambo. Toney haruhusiwi kurejea uwanjani hadi mwishoni mwa Januari, 2024, lakini kwa wakati huo anaweza kuwa rahisi zaidi na kugharimu kiasi kidogo cha fedha.

**#3. Harry Kane**

Kinachofaa zaidi linapokuja suala la washambuliaji wanaoweza kufikiwa katika Ligi Kuu ya England, Harry Kane wa Tottenham Hotspur anaweza kuchukua nafasi ya kuungana na mtu aliyempeleka kwenye safari ya ustaa.

Pochettino anajua jinsi Kane anavyojituma uwanjani na uhusiano wa wawili hao unabaki kuwa thabiti. Huku hali yake akiwa Spurs ikizidi kuwa mbaya, nafasi ya 'kuruka kutoka kwenye meli' inaweza kuwa kubwa mno kwa sana.

**#4. Lautaro Martinez**

Ikiwa mashabiki wa Chelsea wakiwa wakweli, Lautaro Martinez hakuwapo kabisa kwenye orodha ya watu wanaotamaniwa kabla ya Muargentina mwenzake Pochettino kuchukua mikoba ya ukocha.

Kama mambo yalivyokwenda, ukweli ni kwamba Martinez ana kampeni ya kusisimua - labda bora zaidi katika kipindi chake cha uchezaji na kwa namna fulani bado yupo vizuri zaidi.

Mchezaji huyo wa Inter Milan si gwiji wa mbele ambaye mashabiki wengi wanamtafuta, lakini kama unataka mtu ambaye anaweza kuweka mpira wavuni, ni huyu.

**#5. Romelu Lukaku**

Kwa nini usajili mshambuliaji mpya wa pauni milioni 97.5 wakati tayari una mshambuliaji wa pauni milioni 97.5 nyumbani?

Hakuna kingine kinachohitajika kusemwa juu ya kuporomoka kwa uhusiano kati ya mashabiki wa Chelsea na Romelu Lukaku, lakini sasa tuko katika enzi mpya, inaweza kuwa wakati wa kuacha zamani, kuacha mambo ya Italia na kurejea kucheza mpira.

Ukiweza kumvutia Lukaku, yeye ni mmoja wa washambuliaji wachache ambao wanaweza kudai kuwa miongoni mwa watu mashuhuri duniani. Ikiwa Pochettino yuko kwenye vita, hii ndio silaha nzuri zaidi.

Uzuri zaidi ni kwamba kwa Lukaku hakuna fedha inayohitajika ili kumsajili, kwani ni 'mtoto' wao ambaye alipelekwa Inter Milan kwa mkopo na sasa anaweza kurejea nyumbani.

## Nukuu

"Natambua umuhimu wa Ilkay Gundogan, ni mchezaji mzuri na naamini klabu itamalizana naye ili kumfanya aendelee kuwapo hapa, klabu inaangalia namna ya kumpa ofa mpya kuendelea kubaki," **Pep Guardiola akimzungumzia nahodha wake baada ya mchezo wa fainali ya FA dhidi ya Manchester United juzi.**



"Kwangu mimi nadhani nafasi ya golikipa ni tatizo, goli la pili mtu yeyote anaweza kusema lolote, lakini kwangu mimi ni makosa ya golikipa lazima wafanyie kazi," **maoni ya mchambuzi wa soka wa BBC Radio 5, Sutton**




"Real Madrid siku zote itakuwa nyumbani kwake, tunamtakia yeye na familia yake kila la heri katika maisha yake mapya nje ya klabu hii," Kocha wa Real Madrid, Carlo Anncelotti akimzungumzia mshambuliaji **Karim Benzema ambaye atajwa kutaka kuachana na klabu hiyo.**



Nipashe
Spotika

NIPASHE JUMATATU JUNI 5, 2023

# SAFARI YA YANGA HADI FAINALI YA CAF



**Na Adam Fungamwango**

HAIKUTARAJIWA! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga kufika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, ikitolewa kwenye hatua hiyo na USMA ya Algeria kwa tofauti ya mabao ya ugenini.

Juzi, ikiwa kwenye Uwanja wa Juillet jijini Algiers ilishinda bao 1-0, lakini ikalikosa kombe kutokana na kufungwa nyumbani Mei 28 mabao 2-1, hivyo matokeo ya jumla ya kuwa mabao 2-2.

Wenyeji wamenufaika na bao la ugenini kwa sababu wao wamefunga mabao mengi wakiwa ugenini kuliko Yanga.

Awali lengo lilikuwa ni kutinga tu kwenye hatua ya makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika, haikuwezekana.

Ikashuka Kombe la Shirikisho kucheza mechi za mchujo kwa ajili ya kutinga makundi ambayo nayo ilionekana kama ngumu. Lakini iliwezekana. Lengo likabadilika na sasa wakawa wanaitaka robo fainali ya kombe hilo. Baada ya hapo ikawa ni hadithi ya kuvutia hadi kufikia fainali.

Kwenye makala hii, mwandishi anakuletea safari nzima ya Yanga tangu ilipoanzia hadi kutinga fainali ya kombe hilo kwa mara ya kwanza kwenye historia ya klabu hiyo iliyoainishwa mwaka 1935.

**1. Zalan 0-4 Yanga**

Safari ya Yanga mpaka kucheza fainali hiyo juzi ilianza Septemba 10 mwaka jana, ilipocheza hatua ya awali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan ya Sudan Kusini. Ilikuwa ni mechi ya ugenini lakini ikacheza Uwanja wa Banjamin Mkapa na kushinda mabao 4-0.

Straika aliyetwaa kiatu cha dhahabu kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, Fiston Mayele kwa mabao yake saba, alifunga mabao matatu 'hat-trick', moja likiwekwa wavuni na Feisal Salum.

**2. Yanga 5-0 Zalan**

Timu hizo zilirudiana Septemba 17 mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, safari hii Yanga ikiwa mwenyeji, ikishinda mabao 5-0.

Mayele alifunga tena mabao matatu 'hat-trick', mengine yakifungwa na Stephane Aziz Ki na Farid Mussa.

3. Yanga 1-1 Al Hilal

Yanga ilitinga raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika ikapangiwa kucheza dhidi ya Al Hilal ya Sudan. Mechi ilianza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Oktoba 8, timu zote zikitoka sare ya bao 1-1, Mayele akifunga bao upande wa Yanga, Mohamed Yousif akiwafungia wageni.

**4. Al Hilal 1-0 Yanga**

Kipigo cha bao 1-0 ilichokipata ugenini nchini Sudan ikiashiria kushindwa kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo, lakini kapata tiketi ya kucheza mechi ya mchujo kusaka nafasi ya kutinga hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Mechi ilichezwa Oktoba 16, bao likifungwa na yule yule, Yousif.

**5. Yanga 0-0 Club Africain**

Novemba 2 mwaka jana, Yanga ilianza rasmi kampeni yake kwenye Kombe la Shirikisho, ilipocheza mechi ya mchujo dhidi ya Club African ya Tunisia. Ilianzia nchini Tanzania na mechi ikaisha kwa suluhu.

**6. Club Africain 0-1 Yanga**

Katika hali ambayo hakuna aliyetarajia, Yanga ilikwenda kushinda ugenini nchini Tunisia bao 1-0, na kufanikiwa kutinga hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho. Mechi ilichezwa Novemba 9, na bao pekee kwenye mechi hiyo lilifungwa na Stephane Aziz Ki.

**7. US Monastir 2-0 Yanga**

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwenye Kundi D ambalo Yanga iliangukia, ikicheza dhidi ya US Monastir ya Tunisia. Ilifungwa mabao 2-0 ikiwa ugenini Februari 12 mwaka huu, lakini hakukata tamaa.

**8. Yanga 3-1 TP Mazembe**

Iliishushia kipigo cha mabao 3-1, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo Uwanja wa Benjamin Mkapa, Februari 19, kwa mabao yaliyofungwa na Kennedy Musonda, Mudathir Yahaya, na Tuisila Kisinda, Alex Ngonga akiifungia TP Mazembe bao la kufutia machozi.

**9. Real Bamako 1-1 Yanga**

Ilikuwa ni Februari 26 nchini Mali, Yanga ilipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya wenyeji Real Bamako, Mayele akiifungia Yanga bao, Emile Kone akiwasawazishia wageni.

**10. Yanga 2-0 Real Bamako**

Mayele na Jesus Moloko, waliifungia Yanga mabao, iliposhinda 2-0 Machi 8, nchini dhidi ya Real Bamako, ikiendelea kujiwekea vema matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali.

**11. Yanga 2-0 US Monastir**

Ilikuwa ni mechi ya pili mfululizo ikishinda mabao 2-0 nyumbani, pale ilipoinyuka US Monastir ya Tunisia Machi 19, kwa mabao ya Mayele na Musonda.

**13. TP Mazembe 0-1 Yanga**

Ikiwa nchini Congo DR, Yanga iliifunga TP Mazembe nje ndani, safari hii bao 1-0 lililowekwa wavuni na Farid Mussa, pambano likipigwa Aprili 2, mwaka huu.

**14. Rivers United 0-2 Yanga**

Baada ya kuliongoza Kundi D kwa pointi 13, Yanga ilikwenda kucheza robo fainali dhidi ya Rivers United nchini Nigeria, Aprili 23 na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, yote yakitiwa kwenye kamba na Mayele.

**15. Yanga 0-0 Rivers United**

Robo fainali ya pili iliyochezwa jijini Dar es Salaam Aprili 30, timu zote zilitoka suluhu na Yanga kufanikiwa kusonga mbele hatua ya nusu fainali.

**16. Yanga 2-0 Marumo Gallants**

Mechi ya kwanza ya nusu fainali ilicheza nchini, Mei 10, Yanga ikishinda mabao 2-0 yakitiwa kwenye kamba na Aziz Ki na Bernard Morrison.

**17. Marumo Gallants 1-2 Yanga**

Nchini Afrika Kusini, Yanga ilishinda tena mabao 2-1 Mei 17, kwa mabao ya Meyele na Musonda na kuashiria kutinga fainali.

**18. Yanga 1-2 USMA**

Fainali ya kwanza ilicheza Mei 28, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikipoteza mabao 2-1, Aymen Mahious na Islam Merili wakiifungia USM Alger, Mayele akifunga upande wa Yanga.

**19. USMA 0-1 Yanga**

Pamoja na kushinda bao 1-0 ugenini, likifungwa na Djuma Shaaban kwa mkwaju penalti, Yanga imeshindwa kutwaa kombe hilo kwa kanuni ya bao la ugenini. USMA inanufaika kwa kushinda mabao mengi ugenini.

**JE, WAJUA?**



Klabu ya Yanga imecheza fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake mwaka 1935, Fiston Mayele ndiye mchezaji wa kwanza wa ligi ya Tanzania kupewa tuzo ya mfungaji bora wa mashindano hayo kwa mwaka huu.



# Mavunde akazia marufuku mifuko ya plastiki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, amewataka wafanyabiashara nchini kuacha kukwamisha jitihada za serikali za kupinga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo imekuwa na athari kubwa katika uhifadhi wa mazingira.

Mavunde alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kushiriki kufanya usafi wa mazingira jijini hapa ikiwa ni sehemu ya kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Alisema bado kuna wafanyabiashara ambao wamekuwa wakikwamisha jitihada za serikali kukomesha matumizi ya bidhaa za plastiki nchini kwa kuziingiza nchini kinyume na sheria. "Ukiukwaji wa sheria bado unafanywa na wafanyabiashara kwa kuingiza mifuko ya plastini nchini kinyume na sheria zetu na wafanyabiashara wadogo kuendelea kutumia mifuko ya plastiki katika masoko yetu kufungia bidhaa wateja bado ni kikwazo kinachokwamisha jitihada za serikali yetu," alisema Mavunde.

Alisema rai yake kwa wafanyabiashara pamoja na wakazi wa Mkoa wa Dodoma ni kuunga mkono jitihada za serikali kupiga vita matumizi ya mifuko ya plastiki na kushiriki katika kuhifadhi mazingira.

"Moja ya sifa kubwa ya majiji duniani ni usafi wa mazingira Dodoma lazima tuwe wasafi tusisubiri hadi siku za maadhimisho ya mazingira ndipo tufanye usafi, usafi lazima uwe sehemu ya maisha yetu ya kila siku liwe ni jambo la utamaduni wetu sio hadi kulazimishwa na mtu," alisisitiza Mavunde.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Godwin Gondwe, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwataka wanasiasa kuacha kutumia vibaya nafasi zao kuchochea wananchi kuharibu mazingira.

"Maji ya mji wa Dodoma kwa asilimia kubwa yanatoka kwenye msitu wa Chenene hivyo kama wanasiasa wataweka siasa kwenye suala la mazingira tutapata shida sana kwani msitu huu ndiyo unachangia maji ya Mkoa wa Dodoma kwa asilimia 70," alisema Gondwe.

Alisema hivi sasa dunia inakabiliana na mabadiliko tabianchi ambayo yamekuja na athari nyingi ikiwamo kukauka kwa vyanzo vya maji, uhaba wa mvua hali ambayo inachangia mifugo kukosa malisho pamoja na maji.




Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi (kushoto), akimkabidhi zawadi aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA) aliyemaliza muda wake, Prof. Faustine Bee, kwenye hafla ya uzinduzi wa bodi mpya ya mamlaka hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mchengerwa akemea rushwa sekta ya utalii

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ameitaka sekta ya utalii kufanya kazi kwa bidii na weledi ikiwamo kuondoa vitendo vya rushwa ili kuhakikisha kiwango cha fedha za kigeni kinaongeza kutoka asilimia 25 hadi kufikia 50.

Waziri Mchengerewa alisema hayo wakati akizindua mkakati wa kudhibiti ujangili kwenye Hifadhi za Wanyamapori pamoja na wa kitaifa wa kuendeleza hifadhi za Jumuiya ya Wanyamapori za jamii nchini.

Alisema sekta ya utalii hivi sasa inachangia zaidi ya asilimia 25 za fedha za kigeni na kiwango hicho bado ni kidogo kinapaswa kufikia asilimia hizo ili kufikia malengo ambayo wizara imejiwekea.

Alisema jitihada katika utendaji kazi wao wa kila siku zinahitajika, lakini pia kuondoa uzembe kazini na kufanya kazi kwa weledi vitu vitakavyochangia kuongezeka kwa fedha za kigeni kwenye sekta ya utalii hapa nchini.

Alifafanua kuwa watumishi wanapaswa kuendelea kubuni vitu mbalimbali vitakavyoshawishi utalii wa ndani na nje kuongezeka na taifa litazidi kupata watalii wengi.

"Naomba mkafanye kazi kwa bidii katika vitengo vyetu kila mmoja anapaswa kujua kuongeza pato la utalii kwa taifa kwenye sekta ya utalii ni jukumu la kila mmoja hivyo shirikianeni kwenye utendaji kazi," alisema Mchengerwa.

Alisema kupitia eneo hilo wanakazi kubwa ya kufanya hususani kuongeza ubunifu ili kuhakikisha tunatoka asilimia ya chini kufikia ya juu katika eneo lililohifadhiwa kwa ajili ya wanyamapori.

Alisema kuwa yako maeneo ambayo yanapatikana hapa nchinil, lakini duniani huwezi kuyapata, wakiweka wataalamu na kufanya ubunifu uwezekano wa kupandisha kiwango cha utalii upo pamoja na kuongeza pato la taifa katika sekta ya utalii nchini.

Mchengerwa alisema kila mmoja aliyeko nje ya nchi au ndani anapaswa kuitangaza Tanzania kupitia utalii, vyanzo vilivyopo katika maeneo mbalimbali ili kuzidi kuvutia watalii kuja nchini.

Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Maurus Msuha, akizungumzia mkakati huo, alisema hii miwili waliyozindua itasaidia kutokomeza ujangili katika hifadhi za wanyamapori za jamii, pia utachochea kuongeza idadi ya wanyamapori.

Alisema mikakati hiyo itagharimu Dola milion 196,454 huku akisisitiza mikakati hiyo inakwenda kutatua kero kwenye hifadhi za wanyamapori za jamii nchini.

Alisema kwa mwaka 2014-2018 kutokana na mikakati waliokuwa nayo walifanikiwa kuongeza idadi ya tembo kutoka 43,330 hadi kufikia 60,000 na kuongeza kuwa mkakati huu wa sasa wa miaka 10 kuanzia 2023 hadi 2033, wanaamini utafanya kazi vizuri zaidi ya kulinda rasilimali za wanyamapori.

## Wakulima tumbaku waiomba serikali kudhibiti walanguzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

VYAMA vya Ushirika vya Wakulima wa Tumbaku wilayani Manyoni, Halmashauri ya Itigi na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida vimeiomba serikali kuwadhibiti walanguzi kutoka mikoa jirani wanaonunua zao hilo kwa bei ya chini na kuwanyonya wakulima.

Vyama hivyo viliwasilisha kilio hicho juzi wakati wa sherehe ya ufunguzi wa soko la tumbaku msimu wa kilimo wa 2022/2023.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Kanda ya Kati (CEAMCU), Annasia Kimambo, alisema pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na wakulima kuhakikisha zao hilo linawakomboa kiuchumi, changamoto ni kwa walanguzi ambao wananunua tumbaku kwa bei ya chini.

Kimambo, alisema katika msimu wa 2022/2023 Vyama vya Ushirika vya Wakulima wa Tumbaku vinatarajia kupata Sh. bilioni 9.786 kwa kuuza kilo 2,100,000 ikilinganishwa na kilo 406,072 zilizozalishwa katika msimu wa mwaka jana.

Alisema kwa msimu wa 2023/2024 vyama hivyo vitazalisha kilo 4,000,000, lengo la vyama 18 ni kuongeza uzalishaji wa hekta moja kufikia kilo 2,000 badala ya 1,400 zinazozalishwa msimu huu.

Aliongeza kuwa ili kufanikisha kilimo endelevu mpaka sasa vyama vyote 18 vina mabani ya kisasa 6,472 na miti iliyopandwa 807,700 na kila mwaka vimejiwekea mkakati wa kupanda miti 600,000 kila mwaka.

Kaimu Ofisa Tarafa ya Itigi, Eliuta Kidenya, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemilembe Lwota, aliwataka wakulima kutunza mazingira kwa kutengeneza mabani ya kisasa ya kukaushia tumbaku badala ya kukata miti mingi.

Alisema soko la tumbaku liweze kuwa imara wakulima waachane na tabia ya kuchanganya tumbaku na vitu visivyohitajika kuongeza uzito wa kilo.

Baadhi ya wanunuzi akiwamo Fortunata Thadei, Meneja wa kampuni ya MAGEFA na Dukho Myega wa kampuni ya Alliance One, walitoa wito kwa wakulima kuuza tumbaku mapema ikiwa ingali ikiwa na ubora na uzito wa kutosha huku wakipata bonus kwa watakaouza zao hilo kwa kampuni ya Alliance One.

Wakulima waliipongeza serikali kwa kuona umuhimu wa zao hilo katika kukuza pato la taifa pia wao kujikimu na familia zao kupambana na hali ya umaskini.



# Uboreshaji wa sera ya kilimo waongeza tija uzalishaji mazao

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

UBORESHAJI wa Sera ya Kilimo na ongezeko la ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, vimesababisha kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao na kusaidia kuimarika kwa mifumo ya upatikanaji wa chakula nchini.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha wadau wa kilimo na afya jijini Mbeya, Ofisa Kilimo Mkuu kutoka Wizara ya Kilimo, Magreth Natayi, alisema lengo la kikao hicho ni kupambana na hali duni ya lishe mkoani hapo na kuboresha mifumo ya upatikanaji wa chakula.

Alisema kila sekta sera zimeboreshwa na mikakati ya uwekezaji wa kifedha imewekwa ili kuongeza uzalishaji na uboreshaji wa mifumo ya chakula kwa lengo la kuboresha afya za Watanzania.

"Uwekezaji katika sekta ya kilimo umekuwa mkubwa nawahakikishia madiwani, watalaamu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya yale yote yaliyokuwa yamekwama kwenye sekta hii yatatekelezeka kwa sababu bajeti imeongezeka mfano masuala ya kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, huduma za ugani, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na masoko kwa ajili ya wakulima, alisema Magreth.

Akifungua kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka wadau hao kuweka mikakati endelevu ya kuhakikisha mifumo ya upatikanaji wa chakula inaboreshwa.BZAidha, alisema katika kuboresha afya za wananchi maofisa afya kuanzia ngazi ya mitaa, vijiji na kata wameweka utaratibu wa kuwapima watoto wenye umri chini ya miaka mitano uzito ili kujua afya zao namna ya kuwasaidia ili kuepukana na utapiamlo na kutoa ushauri kwa wazazi kuwapatia watoto wao lishe bora.

"Tumeweka mikakati ya kudumu kuboresha mifumo ya chakula, tunashukuru tumejengewa uwezo wa kutosha sasa tunaendelea na utekelezaji wa hii programu ambayo itafika kwenye maeneo yote ya Jiji la Mbeya," alisema Malisa.

Ofisa mradi wa kuboresha mifumo ya chakula katika kukabiliana na matatizo ya lishe katika Jiji la Mbeya, Judith Sarapion, alisema jitihada zilizofanywa na mradi huo kuwa ni kuwajengea uwezo madiwani wa kata zote 36 za jiji hilo kutekeleza afua mbalimbali za lishe.

Alisema kundi hilo ni muhimu kwa sababu wanao ushawishi mkubwa kwenye jamii na kuwa rahisi mpango huo kutekeleza na kufikia malengo waliyojiwekea katika kuboresha afya za wananchi.

Diwani wa Kata ya Itende, Julius Mhaongo alisema watajitahidi kutoa elimu hiyo kwenye vikao vya maendeleo ya kata na kupitia kwenye mikutano ya hadhara ambayo wanatarajia kuanza kuifanya hivi karibuni.



Gari la abiria lililokuwa linatoka Makumbusho kwenda Mbezi likiwa limeingia kwenye mtaro baada ya kudaiwa kusukumwa na lori eneo la Kimara Suka jijini Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa watu walioshuhudia ajali hiyo, walisema baadhi ya abiria walijeruhiwa. **PICHA: HALFAN CHUSI**

## Mahakama yaendelea kusikiliza kesi tuhuma ya kukutwa na jino la tembo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, imeendelea kusikiliza kesi inayomkabili January Tuntuma (31), mkazi wa Kijiji cha Isangawana wilayani Chunya anayetuhumiwa kupatikana na jino la tembo lenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 30.

Shahidi upande wa Jamhuri, askari Emmanuel John wa kituo cha Polisi Chunya mjini, mwishoni mwa wiki aliiambia mahakama kuwa Desemba 4, 2020 saa tano usiku alipigiwa simu ya mkuu wa upelelezi Wilaya ya Chunya akihitajika kazini usiku huo.

Alisema baada ya kufika alimkuta kiongozi huyo akiwa na maofisa wa wanyamapori na mtuhumiwa Tuntuma aliyeelezwa kuwa alikamatwa na nyara ya serikali bila kibali na kuagizwa kuchukua maelezo yake ambaye alikiri kosa na kudai alipata jino la tembo eneo la Luwalaje Chunya ambalo lilithaminishwa kuwa na uzito wa kilogramu tatu na thamani ya Sh. milioni 34.6.

Baada ya maelezo hayo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, George Ngwembe na mwenzake Emelda Aluko, waliiomba mahakama kuahirisha shauri hilo hadi hapo baadaye.

Hata hivyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, aliahirisha kesi hiyo na kusema hadi itakapokuja tena mbele ya mahakama hiyo na mshtakiwa ataendelea kuwa nje kwa dhamana.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa Tuntuma anashtakiwa kwa kosa moja la kupatikana na nyara ya serikali ambayo ni jino la tembo kinyume na kifungu namba 86 (1), (2) (c) (iii) cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori.

# Wakulima 9,000 wapata mafunzo kilimo bora

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

ZAIDI ya wakulima 9,000 wa zao la kahawa, katika mikoa ya Mbeya na Songwe, wamepata mafunzo ya kilimo bora na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuwapatia miche ili kuwasaidia kuzalisha kahawa zenye ubora kwa ajili ya kujiongezea kipato.

Meneja programu wa utafiti wa zao la kahawa kutoka Taasisi ya Utafiti wa zao hilo TaCRI, Kanda ya Mbeya, Dismas Pangalas, alibainisha hayo jana kwenye kikao cha wadau wa zao hilo ambacho kilihusisha mashirika mbalimbali ambayo yanahusika katika kuongeza mnyororo wa thamani.

Alisema jukumu lao ni kutoa mafunzo kwa wakulima na kuzalisha miche bora ya zao hilo na kwa mwaka huu wamewafikia wakulima zaidi ya 9,000 wa mikoa ya Mbeya na Songwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wadau wa Kilimo wasiokuwa wa serikali (ANSAF), Honest Mseri, alisema lengo la kufanya kikao hicho ni kujadili fursa zinazopatikana kwenye zao la kahawa na namna ya kumsaidia mkulima kunufaika.

"Mradi huu unatekelezwa na mashirika matano Café Africa, Brac Maendeleo, Agro Forest, TaCRI na ANSAF ambao unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya ili kuongeza mnyororo wa thamani wa zao hilo kwenye mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma ambao wakulima, maofisa wa kilimo, wafanyabiashara na wadau wa sekta binafsi wamehusishwa katika mpango huu," alisema Mseri.

Alisema kuwa wanajitahidi kuangalia fursa kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji wa zao hilo ili kuliwezesha kundi la vijana na wanawake kujipatia kipato kutokana na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zinazopatikana kwenye kahawa ikiwamo kutengeneza mafuta na vinywaji.

Ofisa Kilimo Mkoa wa Songwe, George Nipwapwacha, alisema kupitia zao hilo fursa nyingi zimepatikana kama vile huduma za kifedha maeneo ya vijijini, biashara za pembejeo za kilimo.

Meneja uzalishaji wa kahawa kutoka Mkoa wa Ruvuma, Rabiel Ulomi, alisema mkoa huo una ardhi kubwa inayofaa kwa kahawa na haijatumika hasa Halmashauri ya Mbinga na Nyasa ambako kuna hekta zaidi ya 6,000.





# Rais Mwinyi akemea wanaCCM wanaotukana viongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema baadhi ya wanachama wa chama hicho wanavunja maadili hawachukuliwi hatua na kutaka watu hao washughulikiwe haraka kwa mujibu wa taratibu za chama.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa CCM ngazi ya mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kichama visiwani humo.

Alisema haiwezekani wanachama wanavunja maadili wanaachiwa na kuzitaka kamati za maadili kutekeleza wajibu wao kwa kukemea wanachama wanaosema maneno ya ovyo dhidi ya chama na kuwatukana viongozi wa juu.

Alisema hali hiyo itasababisha makundi na kuagiza kuitwa na kukanywa ili wajirekebishe na wasiotaka kujirekebisha hatua stahiki zichukuliwe mapema.

Tukiyafanya haya chama chetu kitakuwa na nguvu na wala hakitoweza kushindwa na chama chochote, tusitengeneze ugomvi ndani ya chama," alisema. Alisema hakuna uhai wa chama kama hakutakuwa na umoja na mshikamano.

Aliwataka wanachama kuvunja makundi na kuondoa tofauti zao.

"Hili litatusaidia sana kuhakikisha adui hayumo katika chama tunapambana na maadui wa nje.

Rais Mwinyi alitaka kila kiongozi kujua wajibu na majukumu yake na chama kitafanya mafunzo kwa viongozi wao ili wafanye vizuri katika utendaji wa kazi zote.

Alisema madaftari ya kupigia kura yaliohakikiwa ni nyenzo nzuri ili kuwa na uhakika wa idadi ya wapigakura wingi.

Aidha, alisema kazi ya kutafuta wanachama wapya iwe endelevu kwa kuwa mtaji wa chama cha siasa ni wanachama wapya wanaolipa ada kwa wakati ili kuwa na namba ya kuhakikisha wanashinda katika uchaguzi mkuu.

Akizungumzia uchumi wa chama, alisema kuna baadhi ya ofisi hazina hadhi wala vitendea kazi na kwamba lazima chama kiwe na uchumi na rasilimali nyingi ya kuongezea kipato.

"Tutasimamia uchumi katika chama chetu kwa kuwa na miradi mikubwa ili kumudu gharama mbalimbali ikiwamo za uchaguzi," alisema.

Alisema wakati umefika wa kuwapa posho mabalozi wa chama hicho kwa sababu wanafanya kazi kubwa ndani ya chama. Akizungumzia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, alisema wataekeleza ahadi zote zilizoelezwa katika ilani ya chama hicho.

Alisema ameamua kufanya ziara ili kuimarisha chama na kusimamia ilani ya uchaguzi.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Said Muhammed Dimwa, alisema, chama kimejipanga kujibu hoja za wapinzani.

Alisema serikali imeshatekeleza miradi mingi ya maendeleo ikiwamo kusambaza huduma ya umeme hadi vijiji na kupungua gharama za huduma hiyo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Kusini, Amina Mnacho, akiwalisha taarifa ya chama yenye taarifa mbalimbali ikiwamo utekelezaji wa ilani ya uchaguzi mkoa na hali ya kisiasa ya mkoa.

Alisema chama katika mkoa huo kimeongeza wanachama wapya 400 wakiwamo walitoka chama cha upinzani cha ACT-Wazalendo.




Mke wa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi, akibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa usajili msimu wa nne wa CRDB Bank Marathon katika hafla iliyofanyika Ikulu Zanzibar mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther (wa pili kulia), Mkurugenzi wa Uwekezaji Sanlam, Tullo Mafuru (kulia), Mkurugenzi wa Biashara na Uwekezaji Clouds Media, Sheba Kusaga (wa pili kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa ZMBF, Fatma Fungo (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CAG abaini wizara kushindwa kulipa mil. 553/- boti za uvuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKAGUZI Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, Dk. Othman Abasi Ali, amesema Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, imeshindwa kufanya malipo yenye thamani ya Sh. milioni 552.99 na Dola 934,200 kwa boti za uvuvi na mwani na bidhaa zilizowasilishwa kati ya Juni na Septemba 2022.

Alisema kutokana na kushindwa kukamilisha malipo wizara hiyo ilielekeza matumizi ya fedha kwenye mambo mingine ambayo hayakuwamo kwenye mpango kazi ulioidhinishwa kwa mujibu wa utaratibu jambo ambalo huenda likaisababishia hasara serikali ya kulipa tozo ya fidia inayotokana na ucheleweshaji wa kufanya malipo kwa wakati.

Dk. Abasi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar wakati akiwasilisha ripoti ya CAG ya mwaka 2022 kuwa dosari nyingi zimejitokeza kwa wizara hiyo katika ununuzi wa boti zilizotokana na fedha za UVIKO-19.

Alisema ukaguzi wake umebaini dosari kwa boti zilizotengenezwa kinyume na maelezo ya mikataba ambayo wizara hiyo iliingia mkataba na wauzaji na watengenezaji wa boti zenye urefu na kina maalum.

Alisema amebaini kuwa boti zilizowasilishwa zilikuwa na vipimo tofauti vya urefu na kina ambazo ni kinyume na makubaliano ya mkataba.

"Ukaguzi wangu umebaini upungufu katika urefu na kina cha boti kilichowasilishwa unaathari katika uimara wa boti hizo na uwezo wa kubeba mizigo," alisema. Aidha, alisema dosari nyingine ni kutowasilishwa kwa boti 427 na ukaguzi wake umaebaini hadi kufikia Novemba 2022 makandarasi sita walishindwa kuwasilisha boti hizo kati ya boti 502 za boti zote.

"Kutokana na hali hiyo nimebaini wizara ilisaini hati ya makubaliano Machi 2022 kwa lengo la kupokea boti hizo ifikapo Julai 2022 hadi ukaguzi unakamilika mwezi wa Novemba makandarasi hao walishindwa kuwasilisha boti hizo kwa mujibu wa mikataba," alisema.

Akizungumzia upungufu katika ujenzi wa mabwawa ya samaki, Dk. Abasi alisema wizara hiyo ilisaini makubaliano na kampuni ya Finish Construction kwa ajili ya ukarabati wa mabwawa 10 ya samaki kwa thamani ya Sh. milioni 536.78.

Alisema ukaguzi wake umebaini upungufu katika utekelezaji wa mkataba huo ikiwamo mabwawa matatu yenye thamani ya Sh. milioni 76.84 yalikamilika kwa wakati, lakini wizara ilishindwa kukabidhi mabwawa hayo kwa wakati kwa ajili ya ufugaji wa samaki.

Aidha, alisema kulikuwa na dosari ya mabwawa matatu ya samaki yenye thamani ya Sh. milioni 132.95 ambayo yalitarajiwa kuanza kujengwa Agosti 2022 na hayajaanza kujengwa.

Alisema mabwawa mengine matatu ya samaki yenye thamani ya Sh. milioni 76.84 yalikarabatiwa kinyume na maelezo ya kitaalamu na kusababisha kujitokeza kwa malipo makubwa kinyume na makubaliano ya kazi husika.

Dosari nyingine ni kutoletwa kwa mashine ya kutengenezea chakula cha samaki yenye thamani ya Sh. milioni 139.50.

"Ununuzi wa mashine za boti bila ya ushindani na kufanya manunuzi bila ya kuzingatia ushindani wa bei na kutosambazwa kwa boti 444 na kugaiwa kwa walengwa na kutotumika kwa lengo lililokusudiwa," alisema.

## Mariam Mwinyi azindua msimu wa nne CRDB Bank Marathon

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BENKI ya CRDB kupitia taasisi yake ya CRDB Bank Foundation, imezindua rasmi msimu wa nne wa mbio za CRDB Bank Marathon kwa na lengo la kukusanya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kusaidia kuboresha afya ya mama na mtoto nchini.

Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki wakati wa mazungumzo ya waandishi wa habari na Mke wa Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Zanzibar Maisha Bora Foundation, Mama Mariam Mwinyi, yaliyofanyika Ikulu mjini Zanzibar. Akizindua msimu wa nne wa CRDB Marathon 2023, Mariam aliipongeza Benki ya CRDB kwa msaada wake usioyumba kwa afya ya mama na mtoto kupitia mbio hizo.

Alitoa wito kwa Watanzania kutoka nyanja mbalimbali pamoja na wakimbiaji kutoka nje ya Tanzania, kujiandikisha kwa wingi katika mbio za CRDB Bank Marathon 2023.

Mariam alisisitiza kuwa juhudi za pamoja za washirika na wakimbiaji ni muhimu katika kufikia lengo la kuchangisha fedha kusaidia kutatua changamoto zinazoikabili jamii zilizoainishwa katika malengo ya mbio hizi ikiwamo afya ya mama na mtoto. Alisema kumsaidia mama ni kusaidia jamii nzima na akawataka watu binafsi kuunga mkono jitihada hizo na kuchangia katika mbio hizo.

Katika mahojiano hayo, Mariam alizungumzia wito wake binafsi katika kusaidia jamii uliopelekea kuanzisha Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation yenye lengo la kuboresha maisha ya Wazanzibari kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia zaidi afya ya mama na mtoto.

Alitoa shukrani zake kwa benki hiyo kwa kuchagua kujikita katika sekta ya afya Zanzibar, eneo ambalo linamgusa kwa kuwa ni mdau mkubwa. "Ustawi wa jamii yetu unahitaji kila mmoja wetu kuwa na wito wa kujitoa katika masuala mbalimbali ya kijamii," alisema.

Aliongeza: "Kupitia Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation tunalenga kuinua maisha ya Wazanzibari kiuchumi na kijamii kwa kutilia mkazo zaidi afya ya mama na mtoto. Ninaipongeza Benki ya CRDB na washirika wake kwa kuungana nasi katika kuleta mabadiliko katika sekta ya afya Zanzibar kupitia CRDB Bank Marathon."

Alitumia fursa hiyo pia kutangaza kuwa Dk. Hussein Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, amekubali kuwa mgeni rasmi katika msimu wa nne wa CRDB Marathon 2023. Mbio hizo zimepangwa kufanyika Agosti 13 katika viwanja vya The Green maarufu kama viwanja vya Farasi vilivyopo Oysterbay jijini Dar es Salaam.

# Waziri aipongeza TADB kuisaidia sekta ya maziwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa mchango wake kwa sekta ndogo ya maziwa nchini.

Kiongozi huyo alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la benki hiyo katika maonyesho ya wiki ya maziwa mkoani Tabora.

Ulega alisema Tanzania ni moja kati ya nchi zenye ng'ombe wengi barani Afrika na kusisitiza kuwa uwekezaji wa kimkakati katika sekya ya mifugo utasaidia kuongeza uzalishaji katika mnyororo wa thamani na kuboresha maisha ya wafugaji wadogo na nchi kwa ujumla.

"TADB inafanya kazi nzuri katika kusaidia maendeleo ya sekta ya mifugo pamoja na mnyororo wake wa thamani. Hata hivyo, bado kuna fursa nyingi ambazo hazijatumika katika sekta ya mifugo na hii inaonyesha kuwa bado kuna kazi kubwa inapaswa kufanyika," alisema.

Waziri Ulega alisema wizara yake imeanzisha mradi wa BBT utakaojikita katika mifugo peke yake na kuongeza kuwa mradi huo utafanyika Tabora, moja ya mikoa yenye ng'ombe wengi nchini na kuiagiza TADB kuungana na timu kutoka wizarani kwake kutekeleza mradi huo.

Kaimu Meneja wa TADB Kanda ya Magharibi, Furaha Sichula, alimwambia waziri kuwa TADB kwa kushirikiana na wadau wengine inatekeleza Mradi Shirikishi wa Wasindikaji na Wazalishaji wa Maziwa (TI3P) unaolenga kuwanufaisha wafugaji wadogo 100,000 wa ng'ombe wa maziwa na wachakataji.

Alisema kupitia mradi wa TI3P, TADB na washirika wa mradi, mpaka kufikia hivi sasa wamewezesha uwekazaji wa fedha jumla ya dola za Marekani milioni 7.7 sawa na Sh. bilioni 17 katika kuwasaidia wasindikaji wadogo na wachakataji wa maziwa nchini.

"Moja kati ya mafanikio ya mradi huu ni kuweza kusaidia kifedha katika eneo la mnyororo wa thamani. Jumla ya wakulima 19,124 na wajasiriamali wa wadogo na wa kati wamepatiwa mafunzo ya fedha. Pia wameelekezwa fursa za kifedha zilizopo katika sekta, mahitaji na utaratibu wa kupata mikopo kutoka TADB," alisema.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya I&M Tanzania, Zahid Mustafa (kushoto), akiwa na Shehryan Ali, Meneja Mkuu wa MasterCard Afrika Mashariki, wakati kampuni hizo zilipotiliana saini hati ya makubaliano ya ushirikiano kwenye kadi za malipo ya awali mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aipa kongole Taasisi ya HERI uboreshaji miundombinu shuleni

**Na Prosper Makene, PANGANI**

KATIKA kukuza elimu wilayani Pangani, Taasisi ya HERI Foundation imekabidhi madarasa mawili yaliyokarabatiwa pamoja na madawati mapya 20 na madawati 20 yaliyokarabatiwa kwa Shule ya Msingi Funguni.

Hafla ya kukabidhi miundombinu na samani hizo ilifanyika mwishoni mwa wiki shuleni huko, ikihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainab Abdallah.

Zainab alielezea kufurahishwa na dhamira ya HERI Foundation katika kuleta maendeleo ya elimu wilayani hapa.

Alisisitiza umuhimu wa elimu na nguvu kuwapo miundombinu bora ya kujifunzia. Akaipongeza taasisi hiyo kwa kujitolea kusaidia jamii zisizo na uwezo.

"Ninaishukuru na kuipongeza sana HERI Foundation kwa moyo wenu wa kujitoa kuja kuunga mkono maendeleo ya elimu wilayani Pangani. Ninawaomba mwendelee na moyo huu na muwe walezi wa Shule ya Msingi Funguni. Tunawashukuru sana kwa ukarimu wenu," alisema Zainab. Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya HERI Foundation, Susan Ngole, akielezea dhamira ya shirika hilo, alisema ni farahi kwake kuchangia maendeleo ya Shule ya Msingi Funguni.

"HERI Foundation ina lengo kuu la kuboresha mazingira ya elimu ya kujifunzia na kufundishia. Tumefurahi tumekabidhi madarasa na madawati haya kwani mwanzo yalikuwa katika hali mbaya sana, yasiyoweza kutumika. Ni faraja kwetu kuona sasa wanafunzi wanaweza kuendelea na masomo yao kama kawaida," alisifu.

Hafla hiyo iliashiria hatua kubwa katika safari ya Shule ya Msingi ya Funguni kuelekea kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wanafunzi wake. Mchango huo wa vyumba viwili vya madarasa na madawati utaboresha utowaji wa elimu na kuwawezesha wanafunzi wa Pangani kusoma katika mazingira rafiki.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Funguni, Flora Mayaka, alielezea kufurahishwa na mchango wa taasisi hiyo kwa kusaidia vyumba vya madarasa na madawati vinavyohitajika.

"Leo ni siku ya kipekee kwa shule yetu. Madarasa na madawati haya sio tu yatawapa wanafunzi wetu mazingira mazuri ya kujifunzia, bali pia yatawapa msukumo wa ndoto kubwa na kufikia uwezo wao kamili. Tunaishukuru sana HERI Foundation kwa ukarimu wao katika hili," alipongeza.

Diwani wa Pangani Mashariki, Akida Boramimi, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa taasisi za wadau wa elimu na jamii katika kuinua elimu.

"Mchango huu ni matokeo ya juhudi za pamoja za serikali na taasisi kama HERI Foundation. Inatia moyo kushuhudia ushirikiano kama huu unafanya kazi kwa lengo moja - kuboresha ubora wa elimu Pangani. Tuendelee kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya kuboresha elimu kwa watoto wetu," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Rajabu Rajabu, akitoa shukurani kwa niaba ya wazazi na wanakijiji, alisema: "Tumefurahishwa na mchango wa HERI Foundation katika Shule ya Msingi ya Funguni. Watoto wetu wanastahili elimu bora na kwa madarasa haya na madawati, tunaweza kuwahakikishia mustakabali mwema. Tunashukuru kwa dhati kwa mchango huu."

Hafla hiyo ilihitimishwa kwa kikao kifupi cha tathmini ya mradi huo wa ukarabati wa madarasa na madawati kati ya watendaji wa Shule ya Msingi Funguni na wafanyakazi wa HERI Foundation ili kuboresha utendaji kazi kwa miradi ijayo.

Shule hiyo ilianzishwa mwaka 1976. Kwa sasa ina wanafunzi 668 na walimu 18. Pia ina darasa la elimu maalum kwa watoto wenye ulemavu wa akili (Intellectual Impairment).

Inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu kama vile madarasa, madawati, vyoo, majiko na ukosefu wa bwalo kwa ajili ya chakula cha wanafunzi. Pia kuna uhaba mkubwa wa nyumba za walimu na zilizopo zinahitaji ukarabati mkubwa. Zinavuja na ni chakavu zisizo na maji wala umeme.


## KUPOTELEWA NA CHETI



**HAMADI J. STIMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. S0496-233 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **JITEGEMEE SECONDARY SCHOOL** Mwaka 1990. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: URP/RB/9813/2005.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JUMA SHABANI CHAYE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina la **MOSES JOSEPH MINJA** yenye namba ya usajili **T 572 DJN** aina ya **TOYOTA KLUGER.** Chassis namba **ACU200039390** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/189062/2023.**

# Kituo chaita wadau kusaidia mahitaji ya watoto yatima

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha kulelea watoto cha Hisani Orphanage Center cha Kigamboni jijini Dar es Salaam, kimeomba jamii kupeleka misaada katika kituo hicho chenye watoto 71 wenye mahitaji mbalimbali.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa kituo hicho, Idaya Mutalemwa, alipopokea msaada wa vyakula mbalimbali kutoka kwa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Alisema mahitaji makubwa ni chakula kutokana na idadi kubwa ya watoto wanaolelewa katika kituo hicho ambao wengi walichukuliwa baada ya wazazi wao kufariki na kukosa watu wa kuwatunza.

"Mahitaji makubwa hasa ni chakula kwa sababu ukiangalia idadi hii ya watoto ni kubwa sana. Magodoro pia hayatoshelezi na pia kodi ya nyumba tunalipa Sh. milioni 3.6 kila baada ya miezi sita lakini wakati mwingine tunaikosa," alisema Idaya.

"Tunaomba mtu atakayejitolea tuwe na makazi ya kudumu ili tuondokane na kutangatanga mara leo tuko Mbagala kesho tuko Kigamboni ili tuwalee watoto hawa katika mazingira mazuri. Tunashukuru CBE kwa kuja kutushika mkono, watoto wamefarijika sana," alisema.

Waziri wa Wanawake na Jinsia wa CBE, Elizabeth Obadia, alisema waliamua kwenda kutoa msaada huo kutokana na kituo hicho kuwa na mahitaji makubwa hasa ya chakula na mavazi.

"Sisi ni chuo cha umma, tuna kila sababu ya kuchangia taasisi kama hizi zinazolea watoto wenye mahitaji kama hawa ambao kwa kweli tumewakuta katika mazingira magumu na tunaomba jamii iwe inakumbuka kwenda katika vituo kama hivi," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kujenga utamaduni wa kusaidia wenye mahitaji kama watoto wanaolelewa katika vituo hivyo ili na wenyewe wajisikie kwamba ni sehemu ya jamii na kuishi maisha mazuri.

Mmoja wa watoto wanaolelewa katika kituo hicho, Rahma Mshamu, alisema amehitimu kidato cha nne na anatarajia kujiunga na kidato cha tano lakini hana fedha za kumwezesha kununua mahitaji mbalimbali.

"Nimepata daraja la pili. Kwa hiyo, ninaomba msaada ili nifike mbali kielimu kwa sababu mlezi wetu hapa hawezi kutimiza mahitaji yetu yote. Hapa mlezi wetu amepanga, analipa kodi. Kuna mahitaji ya maji, umeme na hawezi kulipia mahitaji yote," alisema.

Rahma ambaye alihitimu kidato cha nne mwaka jana katika sekondari ya serikali Nzasa, alisema wazazi wake wote walifariki dunia akiwa na umri mdogo na ndipo alipopelekwa katika kituo hicho cha kulelea yatima.

# Hakuna manusura wengine ajali treni

**NEW DELH, India**

MAMLAKA za India zimesema waokoaji hawajafanikiwa kuwapata watu wengine walionusurika katika ajali iliyohusisha treni mbili za abiria na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 280.

Mamia ya watu wamejeruhiwa katika ajali hiyo iliyotokea usiku wa kuamkia juzi, ikitajwa kuwa mbaya zaidi kuwahi kutokea India.

Treni hizo ni Coromandel Express iliyokuwa inatoka Howrah, Jimbo la Bengali Magharibi kuelekea Chena, Jimbo la Tamil Nadu, na Howrah Superfast Express iliyokuwa inatoka Bengaluru huko Karnataka kuelekea Howrah.

Ilielezwa kuwa waokoaji walilazimika kupanda juu ya mabehewa ya treni yaliyoharibiwa na ajali wakivunja milango na madirisha ili kuwaokoa watu waliokuwa ndani.

Mamlaka za uokoaji zilisema idadi ya vifo iliongezeka usiku kucha na miili ya waliofariki dunia iliyofunikwa mashuka meupe ililazwa chini karibu na njia ya reli huku wenyeji wa eneo wakiwasaidia walionusurika.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Dharura na Zimamoto wa Jimbo la Odisha, Sudhanshu Sarangi, alisema kufikia saa nne usiku wa ajali, walifanikiwa kuwaokoa watu walionusurika na baada ya hapo shughuli iliyofuata ilikuwa ya kuitoa miili.

Mamlaka zilieleza kuwa mbali na vifo 280, pia kulipatikana majeruhi 900 wakati uchunguzi wa chanzo cha ajali hiyo unaendelea.

Kwa mujibu wa Ofisa Mwandamizi wa India Jena, kati ya majeruhi hao, waliojeruhiwa vibaya ni 200 na wengine 200 waliruhusiwa kutoka hospitalini baada ya kupatiwa matibabu, na raia wengi walijitokeza kutoa damu ili kuyanusuru maisha ya majeruhi.

Jena alisema wakati shughuli za uokoaji zikielekea ukingoni, moja ya changamoto kubwa hivi sasa ni kuitambua miili ya waliopoteza maisha katika ajali hiyo.

Alieleza kwamba ndugu wa marehemu watapatiwa miili ya ndugu zao pale watakapofanikiwa kuthibitisha kwa ushahidi uhusiano wao na baada ya miili kufanyiwa uchunguzi, akieleza kuwa huenda vipimo vya vinasaba (DNA) vikatumika ili kufanya utambuzi.

Msemaji wa Wizara ya Reli, Amitabh Sharma, alisema mamlaka za reli zitaanza kuondoa mabaki ya treni zilizohusika kwenye kisa hicho ili kufanya matengenezo ya reli na kuruhusu kuendelea kwa safari za treni.

Mwezi Agosti 1995, treni mbili ziligongana karibu na mji mkuu wa New Delhi na kusababisha vifo vya watu 358 ikiwa ni kati ya ajali mbaya India.

Mwaka 2016, treni ya abiria iliteleza na kuacha njia yake katikati ya miji ya Indore na Patna na watu 146 walifariki dunia, na kwamba makosa ya kibinadamu na vifaa vya kutolea ishara vilivyopitwa na wakati ndivyo vinavyolaumiwa kusababisha ajali nyingi kati ya hizo.

*DW*




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Herman Kasekende (wa pili kushoto), akiwangoza baadhi ya wafanyakazi wa benki hiyo kufanya usafi katika ufukwe wa Kibo jijini Dar es Salaam juzi katika kaulimbiu ya BeatPlastic kuelekea Siku ya Mazingira Duniani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# EAC yakubali kuondoa vikwazo 10 vya forodha

**Suzan Mshakangoto na Benny Mwaipaja, WFM**

NCHI Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zimekubaliana kuondoa vikwazo 10 vya kibiashara visivyo vya kiforodha (NTB), huku vikwazo vinane vikiendelea kushughulikiwa.

Vilevile, vikwazo vingine vipya vinne vimewasilishwa ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara baina ya nchi hizo.

Nchi hizo pia zimekubaliana kutoza kiwango cha dola 10 za Marekani kwa kilomita 100 kwa ajili ya matumizi ya barabara (road user charge) kwa magari ya mizigo kutoka nchi moja kwenda nyingine katika jumuiya badala ya kila nchi kuwa na viwango vyake vya tozo.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika Mkutano wa 42 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji la Jumuiya ya Afrika Mashariki (SCTIFI) uliofanyika juzi katika Makao Makuu ya Jumuiya jijini Arusha.

Wakizungumza baada ya mkutano huo, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, walisema baraza hilo limekubaliana kutoza dola 10 za Marekani kwa kilomita 100 kwa ajili ya matumizi ya barabara kwa malori ya mizigo yanayofanya safari katika nchi wanachama badala ya kila nchi kutoza gharama zake, pamoja na kuimarisha utoaji huduma za forodha katika mpaka wa Kenya na Tanzania. Kutapunguza msongamano wa malori na kuchochea ukuaji wa biashara.

Pia walisema baraza limekubaliana kuondoa gharama ya viza kwa watu wanaotaka kusafiri kutoka nchi moja kwenda nyingine kwa shughuli mbalimbali zikiwamo za kibiashara, ili kukuza uhusiano miongoni mwa wakazi wa jumuiya hiyo pamoja na kuchochea ukuaji wa biashara na uchumi wa nchi husika.

Kuhusu uondoshaji wa mizigo, mawaziri hao walifahamishwa kuwa mizigo ya Tanzania inayosafirishwa kwenda Kenya itaendelea kuondoshwa kupitia Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha ulioanza kutumika kuanzia mwezi Aprili mwaka huu.

Mkutano huo pia umeidhinisha Rasimu ya Mwisho ya Viwango vya Afrika Mashariki (FDEAS) ambapo viwango 65 vitaanza kutumika rasmi, umepitisha Andiko la Kisera kwa ajili ya EAC kufanya majadiliano na maeneo mengine ya kikanda na nchi nyingine, pamoja na hadidu za rejea kwa ajili ya kuandaa Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi ya EAC. Pia hadidu za rejea kwa ajili ya kuandaa mkakati wa mamlaka za ushindani kwa kipindi cha mwaka 2024-2029.

Mkutano huo pia umepitisha kutumika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa EAC wa utoaji wa taarifa na utatuzi wa vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha (NTB) ujulikanao kama NTB App.

Pamoja na makubaliano hayo, mkutano huo pia ulipokea na kujadili taarifa ya mashauriano ya awali ya bajeti ya mawaziri wa fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

HABARI MICHEZO

# SANAA MORO YATAKIWA KUELIMISHA JAMII

**Na Ashton Balaigwa,**

MOROGORO

TASNIA ya Sanaa mkoani Morogoro, imetakiwa kuhakikisha inafanya kazi zake za kuelimisha jamii na namna ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto pamoja na kutoa elimu ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwenye jamii ikiwamo ndoa za jinsia moja.

Agizo hilo limetolewa na Ofisa Michezo na Utamaduni Mkoa wa Morogoro, Grace Njau, wakati akizindua Mtandao wa Maendeleo ya Sanaa na Utamaduni (TAGOSINE) mkoa wa Morogoro lengo lake kuunganisha washiriki wote wa tasnia hiyo ili kuwa na nguvu ya pamoja.

Njau alisema moja ya faida ya sanaa ni pamoja na kusaidia nchi katika kuhamasisha na kuleta amani na utulivu pamoja na kupiga vita mambo yanayopingana na tamaduni za hapa nchini ikiwamo mapenzi ya jinsia moja na vitendo vya ukatili.

Alisema tangu serikali ya awamu ya sita kuingia madarakani imekuwa ikithamini sana tasnia hiyo na kutoa kipaumbele katika mambo mbalimbali kutokana na umuhimu wake wa kuendeleza tamaduni mbalimbali za hapa nchini kupitia sanaaa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Taifa wa Taasisi ya Maendeleo ya Sanaa Tanzania (TAGOSINE) David Msuya, alisema taasisi hiyo inalenga kuhakikisha inatangaza miradi yote inayofanywa na serikali ya Tanzania pamoja na kulitetea taifa kupitia sanaa.

Msuya alisema pia taasisi hiyo imelenga kuendeleza sekta filamu na uigizaji, sanaa na maonesho, muziki pamoja na sanaa ya ufundi ambapo wahusika watasaidiwa kufanya sanaa zao na kutafutiwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo alisema pamoja wasanii hao kusaidiwa lakini TAGOSINE Taifa itaanzisha tawi la Chuo cha Sanaa Morogoro kwa ajili ya kuibua vipaji mbalimbali ili kuongeza wasanii katika fani mbalimbali.

Alisema chuo hicho kitatoa mafunzo bure kwa watu watakaibuliwa katika vipaji mbalimbali na wataunganishwa na taasisi mbalimbali kuweza kufanya sanaa zao bila vipingamizi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TAGOSINE mkoa wa Morogoro, Abdulaziz Salehe, akiongea baada ya kusimikwa nafasi hiyo, alisema kazi kubwa atakayofanya ni kuhakikisha kazi zote za sanaa zinazofanywa mkoani humo zinatambulika na kusimamiwa masoko yake ili msanii aweze kunufaika kupitia jasho lake.



Wachezaji wa mpira wa kikapu, Yohana John (kulia) na Innocent Limo, wakiwania mpira walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dr es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dula Mbabe kupanda ulingoni Julai 15

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Abdala Pazi (Dula Mbabe) anatarajiwa kupanda ulingoni Julai 15 mwaka huu kupigana na Eric Tshimanga Katompa kwenye pambano litakalofanyika jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, promota wa pambano hilo Meja Selemani Semunyu alisema maandalizi yanaendelea vizuri na kwa asilimia kubwa yamekamilika.

"Pambano hilo litakuwa la kihistoria kwani mabondia ambao wanakwenda kukutana ni wenye viwango na Watanzania pamoja na wadau wa ngumi watarajie burudani siku hiyo," alisema Semunyu.

Aidha, alisema kutokana na maandalizi hayo anaamini kila kitu kitakwenda sawa hivyo mashabiki wajiandae kwa burudani.

Semunyu alisema mbali na pambano hilo pia kutakuwa na mapambano ya utangulizi ambayo yatavuta hisia za wadau wa mchezo huo.

"Moja ya mapambano ya utangulizi ni lile la Hassan Ndonga ambaye atapigana na James Kibazange, kiufupi ni siku ya burudani kwa wadau wa mchezo wa ngumi," alisema Meja Semunyu.

Alisema mapambano hayo yatatoa burudani kwa wadau na mashabiki wa mchezo wa ngumi hivyo wasikose kuhudhuria.

## Meridianbet yaja na mpya

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya michezo ya kubashiri ya Merianbet imekuja na mchezo mpya wa kasino mtandaoni unaojulikana kwa jina la 'Poxer exas Hold'em' unaolenga kuwapitia mkwanja wachezaji wake.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet, Matina Nkurlu, amesema mchezo huo utatoa fursa kwa wateja wanaocheza kuvuna pesa.

Akizungumza na Nipashe jana, Nkuru alisema kutokana na ligi nyingi kubwa za soka duniani kuisha kwa msimu huu wamekuja na mchezo huo kuwapa fursa wachezaji wake kuendelea kuvuna pesa.

Alisema mchezo huo wa Poker Texas Hold'em ni moja kati ya michezo itayoenda kung'arisha msimu mpya kwa kukupata mkwanja wa kutosha, kuanzia Juni 2 mpaka Juni 26.

"Poker Texas Hold'em ni mchezo wa karata unakupa nafasi ya kuchagua aina gani ya karata itatokea, kwenye mchezo huu utapewa karata mbili mkononi mwako na zingine 5 zinakuwa ni karata za pamoja ili kufikisha idadi ya karata 5 katika hatua 3 tofauti," alisema Nkurlu.

## JKT Queens yajipanga mashindano Majeshi

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya soka ya JKT Queens imeanza kujinoa kwa ajili ya mashindano ya Majeshi yanayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Juni 31, mwaka huu nchini Uholanzi.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Kocha wa timu hiyo, Ally Ally, alisema kikosi chake kina morali ya juu kuelekea kwenye mashindano hayo ambayo yatashirikisha timu za majeshi kutoka nchi mbalimbali.

"Tunajipanga vizuri kuhakikisha tunakwenda kuiwakilisha na kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye mashindano hayo tunaomba Watanzania watuunge mkono, alisema Ally.

Alisema kutokana na mazoezi anayowapa wachezaji wake ana uhakika wa kufanya vizuri na kurudi na ubingwa kwenye michuano hiyo.

Kwa upande wake ofisa habari wa timu hiyo, Sajini Elizabeth Buliba, alisema timu hiyo itaondoka nchini kati ya Juni 25-27 kuelekea nchini humo.

Alisema kabla ya kuelekea Uholanzi watacheza mchezo mmoja wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya timu ya Taifa ya Zambia Juni 10, mwaka huu nchini Zambia.

## ZISIKUPITE

### GUNDOGAN KUTUA BARCA

NAHODHA wa Manchester City, Ilkay Gundogan yuko mbioni kujiunga na Barcelona mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa joto, huku klabu hiyo ya LaLiga ikimshawishi kiungo huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 32 kwa ofa ya mkataba wa miaka mitatu. ***(Sport)***

### KOVACIC KARIBIA CITY

CHELSEA itadai ada ya takribani pauni milioni 35 kwa kiungo wao wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic mwenye umri wa miaka 29, ambaye anaonekana kukaribia kuhamia Manchester City. ***(90 Min)***

### RICE SAFI ARSENAl

ARSENAL imefikia makubaliano ya kibinafsi na kiungo wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24. ***(FootballTransfers)***

### BAYERN WAKOMAA NAYE

KLABU ya Bayern Munich haijakata tamaa ya kumsajili Declan Rice kutoka West Ham baada ya kukutana naye jijini London, huku mabingwa hao wa Ujerumani wakipanga kuandaa ofa rasmi. ***(Sky Sport)***

### MOYES KUFUTWA KAZI

KLABU ya West Ham huenda ikamfuta kazi kocha wao David Moyes ikiwa hawatashinda fainali ya Ligi ya Europa Conference dhidi ya Fiorentina Jumatano. ***(Guardian)***

### MAGUIRE CHAMBO KWA MOUNT

MANCHESTER United itamtoa mlinzi wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30 kwa Chelsea kama sehemu ya mabadilishano na kiungo wa kati, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

### VLAHOVIC KUHAMA

BAYERN Munich na Manchester United bado zinavutiwa na mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 23, ambaye yuko tayari kuhama msimu huu ikiwa Massimiliano Allegri ataendelea kuwa kocha wa Juventus kwa sababu ya uhusiano wao mbaya. ***(Nicolo Schira)***

### ALLISTER KUACHIWA

LIVERPOOL imekubali kufikia kipengele cha kuachiliwa kwa Alexis Mac Allister na watailipa Brighton ada ya pauni milioni 55 kwa kiungo huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

### CAICEDO AWANIWA CHELSEA

CHELSEA inatazamia kumleta mchezaji wa kimataifa wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21 kutoka Brighton na mchezaji wa kimataifa wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 22, kutoka Sporting Lisbon ili kuboresha safu yao ya kiungo. ***(Guardian)***

### MESSI NA BARCA

BARCELONA ina imani kwamba Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga itaidhinisha mipango yao ya kifedha hivi karibuni, ili kuwawezesha kuanza mpango wao wa uhamisho, ambao utajumuisha kusajiliwa tena kwa mshambuliaji wa Argentina mwenye umri wa miaka 35 na gwiji wa klabu hiyo, Lionel Messi kwa uhamisho wa bure kutoka Paris St- Germain. ***(90 Min)***

### BENZEMA KUMALIZA MKATABA

KARIM Benzema atakamilisha mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Real Madrid, licha ya tetesi kuwa mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 35, yuko tayari kukubali ofa kubwa ya kuhamia Saudi Arabia msimu huu wa joto. ***(Marca)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAMOS RASMI KUONDOKA PSG

**PARIS, Ufaransa**

SERGIO Ramos ataondoka Paris Saint-Germain baada ya mchezo wao wa mwisho wa msimu jana Jumamosi, mchezaji na klabu walithibitisha.

Mkataba wa Ramos unaotarajiwa kumalizika msimu huu wa joto na hautaongezwa tena na hivyo kumfanya apatikane kwa uhamisho wa bure.

"Nimeaga na sasa nafuata hatua nyingine ya maisha yangu, kwaheri PSG," aliandika Ramos kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii.

"Sijui ni sehemu ngapi mtu anaweza kujisikia yuko nyumbani, lakini bila shaka PSG, mashabiki na Paris walikuwa wapo pamoja na mimi.

"Asante kwa miaka miwili maalum ambayo niliweza kucheza katika kila mashindano na kujitolea. Nitakabiliana na changamoto mpya, nitavaa rangi nyingine."

Naye Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa PSG, Nasser Al-Khelaifi katika taarifa yake alisema: "Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Sergio Ramos kwa miaka miwili ambayo amekaa nasi.

"Uongozi wa Sergio, ari ya timu na kiwango chake, pamoja na uzoefu wake katika kiwango cha juu, vinamfanya kuwa gwiji wa soka wa kweli, na ilikuwa heshima kuwa naye Paris. Kila mtu katika klabu anamtakia kila la heri."

Ramos mwenye umri wa miaka 37 alijiunga na PSG msimu wa joto wa 2021 baada ya kukaa kwa miaka 16 Real Madrid, ambapo alishinda mataji matano ya LaLiga na mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshindi wa Kombe la Dunia 2010 akiwa na Hispania, mlinzi huyo alicheza mechi 57 na kushinda mataji ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, katika misimu yake yote miwili akiwa PSG, lakini klabu hiyo ilishindwa kufuzu hatua ya 16 bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kufuatia msimu mwingine wa kukatishwa tamaa kwenye mashindano ya Ulaya, PSG inatarajiwa kufanyiwa mabadiliko makubwa msimu huu.

Kocha wa PSG, Christophe Galtier alithibitisha Alhamisi kwamba Lionel Messi pia ataondoka mkataba wake utakapomalizika msimu huu wa joto, wakati vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Neymar naye yupo tayari kuondoka.

Ramos pia alitangaza kustaafu kuichezea timu ya taifa ya Hispania Februari baada ya kucheza mechi 180.

Mbali na Kombe la Dunia, alishinda kombe la Ulaya mwaka 2008 na 2012.

PSG, ambao walitwaa ubingwa wa Ligue 1 wikendi iliyopita, walicheza mchezo wao wa mwisho wa msimu huu wakiwa nyumbani dhidi ya Clermont Foot Jumamosi.

# MOURINHO ASHTAKIWA KUMTUSI MWAMUZI



**ROME, Italia**

SHIRIKISHO la soka Ulaya, UEFA, limelaani kunyanyaswa kwa mwamuzi wa fainali ya Ligi ya Europa, Anthony Taylor na familia yake na mashabiki wa AS Roma, huku kocha wa klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Jose Mourinho akishtakiwa kwa kutumia lugha ya matusi dhidi ya ofisa huyo wa mechi.

Taylor alianza kushutumiwa na kutishwa baada ya Roma kupoteza kwa changamoto ya mikwaju ya penalti dhidi ya Sevilla kwenye fainali Jumatano.

Mechi ilikuwa tete huku Taylor akiwa ametoa kadi za njano 14, zikiwa ndio kadi nyingi zaidi kuwahi kutolewa katika mchezo wa Ligi ya Europa.

Siku moja baada ya mechi, video zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii zikimwonyesha mwamuzi huyo wa England Taylor na familia yake wakinyanyaswa na mashabiki wa Roma kwenye Uwanja wa Ndege wa Budapest.

Katika video hiyo, mashabiki wa Roma walionekana wakimtusi Taylor mwenye umri wa miaka 44 na familia yake, ambao walilazimika kupewa ulinzi kwenye uwanja wa ndege.

"UEFA inalaani vikali tabia ya vurugu inayoelekezwa kwa mwamuzi wake Anthony Taylor na familia yake. Vitendo kama hivyo havikubaliki na vinadhoofisha roho ya uchezaji wa haki na heshima ambayo UEFA inasimamia," ilisema taarifa ya UEFA.

"UEFA inadumisha ushirikiano wa karibu na polisi wa ndani na usalama wa uwanja wa ndege kuanzia waamuzi kuwasili katika miji waandaaji.

"Hata hivyo, tunajitahidi kila mara kuimarisha hatua za usalama kwa maofisa kwa uratibu na mamlaka. Tutatathmini matukio kwa makini na kujumuisha maarifa muhimu katika michakato yetu ya kupanga matukio ya siku zijazo."

Kama sehemu ya taratibu za kinidhamu baada ya fainali hiyo, shirikisho la soka barani Ulaya siku ya Ijumaa lilimshtaki Mourinho, ambaye alirekodiwa akiwatolea maneno ya kashfa maofisa nje ya uwanja wa Puskas Arena.

Kocha huyo raia wa Ureno alimkosoa mwamuzi katika maoni yake baada ya mchezo, akisema, "ulikuwa mchezo mkali, wa kiume na wa kusisimua na mwamuzi ambaye alionekana Mhispania. Ilikuwa ya njano, njano, njano wakati wote."

Mashabiki wa timu zote mbili pia wameshtakiwa kwa kufyatua fataki na kurusha vitu, huku mashabiki wa Roma wakidaiwa kufanya uharibifu pamoja na fujo.

Sevilla pia wameshtakiwa kwa kuvamiwa uwanjani na mashabiki wao, ambao walitoka mbio hadi uwanjani baada ya Gonzalo Montiel kufunga bao la ushindi.

# Lingard atemwa kikosi cha Forest

**LONDON, England**

JESSE Lingard anaongoza orodha ya nyota sita waandamizi ambao hawataongezewa mikataba yao na Nottingham Forest.

Kiungo huyo wa zamani wa Manchester United mwenye umri wa miaka 30, aliwasili hapo kwenye Uwanja wa City Ground msimu uliopita wa joto na akafanywa kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika klabu hiyo, lakini amekuwa na wakati mgumu wa kuanza kwenye kikosi cha Kocha Steve Cooper.

Akiwa ameanza katika mechi 12 pekee na tano akitokea benchi kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, Lingard atakuwa mchezaji huru baada ya kumalizika kwa mkataba wake wa sasa baadaye mwezi huu.

Kuna hakika kutakuwa na ofa kwa mzaliwa wa Warrington, ambaye alicheza mechi 232 katika mashindano yote akiwa na Mashetani Wekundu na alipelekwa kwa mkopo West Ham katika kipindi cha pili cha msimu wa 2020-21.

Lyle Taylor, Jack Colback, Andre Ayew, Jordan Smith na Cafu wote wanaelekea kwenye mlango wa kutokea pamoja na mchezaji huyo wa kimataifa wa England aliyeichezea nchi hiyo mechi 32.

Mshambuliaji Chris Wood pia atashuhudia uhamisho wake wa mkopo wa Januari kutoka Newcastle ukifanywa kuwa wa kudumu.

Forest walikosolewa sana kwa sera ya uhamisho ambapo ilisajili wachezaji wapya 22 msimu uliopita wa joto na wakafanikiwa kubaki Ligi Kuu kwa pointi nne.

# Real Madrid yamfukuzia Havertz

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid inamfukuzia mchezaji wa Chelsea raia wa Ujerumani, Kai Havertz katika dirisha hili kubwa majira ya joto ili kuhakikisha wanaimarisha kikosi chao katika safu ya ushambuliaji.

Real Madrid inahitaji mshambuliaji mwingine ili kuboresha timu hiyo kwenye safu ya ushambuliaji na Havertz ameingia kwenye orodha ya wababe hao wa soka nchini Hispania.

klabu hiyo inafikiria kutuma ofa kwa klabu ya Chelsea kwa ajili ya kumpata mchezaji huyo huku Chelsea ikiwa tayari kumwachia mshambuliaji huyo.

Klabu hiyo imeweka bayana kuwa itamuuza jumla na suala la kutolewa kwa mkopo sio kipaumbele chao hivo wako tayari kusikiliza ofa kwa klabu ambazo zitakua zinamtaka mchezaji huyo.

Real Madrid wao watatuma ofa kwa klabu ya Chelsea lakini inafahamika kuwa klabu hiyo haipo tayari kutoa dau kubwa kumnunua mshambuliaji huyo, kwani mchezaji pekee ambaye wamepanga kumsajili kwa gharama kubwa ni kiungo wa kimataifa wa England, Jude Bellingham ambaye anakipiga kule Borussia Dortmund.

Taarifa za mshambuliaji Karim Benzema kuondoka klabuni hapo na kutimkia Saudia Arabia zimeifanya klabu hiyo kuanza kutafuta mshambuliaji mwingine haraka.



# COASTAL UNION YAIPANIA AZAM FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Coastal Union, Fikirini Elius, amesema mchezo wao dhidi ya Azam FC ni mchezo muhimu utakaowahakikishia nafasi ya kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Coastal inatarajiwa kuwakaribisha Azam FC Juni 6 kwenye uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

"Kikosi changu kipo imara kuivaa Azam na tuna uhakika wa kupata pointi tatu, tumekuwa tukifanya mazoezi hasa ya utimamu wa mwili kwa sababu tunachoangalia ni ukubwa na ubora wa Azam na wachezaji waliokuwa nao, hivyo sisi inabidi kujiandaa mara mbili zaidi yao," alisema kocha huyo.

Alisema kuwa ni mchezo muhimu na wachezaji wake wameonyesha morali ya hali ya juu kuelekea kwenye mchezo huo.

"Tunaiheshimu Azam, ni timu kubwa na inawachezaji wenye uwezo mkubwa, lakini hiyo si sababu ya kuwaogopa, tunaandaa timu kwa ajili ya kushindana nao, wachezaji wangu wanatambua umuhimu wa michezo yetu miwili iliyobaki ukiwamo mchezo huu wa Azam," alisema Elius.

Coastal Union inashika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 33 mpaka sasa, lakini bado haimpi uwezekano wa moja kwa moja kutoshuka daraja au kwenda kucheza 'play off'.

Timu hiyo ina kazi ngumu kwani imebakisha mechi mbili na timu ambazo ni vigogo vya soka, Juni 6 ikitarajia kucheza dhidi ya Azam na Juni 9 ikitarajia kumaliza msimu wa Ligi Kuu 2022/23 ikicheza dhidi ya Simba.



Mchezaji wa Timu Soka ya Bulls, Ben Mango, akiwatoka mabeki wa Under Future Star, kwenye mashindano ya Dar Youth Cup chini ya miaka 13 yanayofanyika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Yanga kula 'msosi' na Samia Ikulu

INATOKA UK. 24

Licha ya ubao kusomeka mabao 2-2, Yanga imeshindwa kutwaa kombe hilo kutokana na kanuni ya bao la ugenini, huku wenyeji USMA wakinufaika kushinda mabao mengi wakiwa ugenini kuliko wawakilishi hao wa Tanzania.

Pamoja na kwamba Yanga haikutwaa kombe hilo, wachezaji wake, benchi la ufundi na viongozi wamevishwa medali ya fedha huku mshambuliaji wake Fiston Mayele akitwaa kiatu cha ufungaji bora wa michuano hiyo akiwa na mabao saba, golikipa Djugui Diarra alipewa tuzo ya mchezaji bora wa mechi hiyo ya mkondo wa pili wa fainali ya Kombe la Shirikisho.

Aidha, Rais wa Yanga, Hersi Said, ameitoa medali yake ya michuano hiyo kwa Rais Samia, akisema yeye ndiye amekuwa chachu ya wao kufika walipofika kutokana na hamasa kubwa aliyokuwa akitoa tangu kuanza kwa michuano hiyo.

"Medali hii naipeleka kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yeye amekuwa sababu kubwa ya sisi kufika hapa, ametusaidia mambo mengi, hamasa, mwongozo hadi leo tumefika hapa," alisema.

Akizungumzia mechi hiyo alisema ilikuwa nzuri na ngumu yenye hadhi ya kuitwa fainali.

"Ilikuwa mechi nzuri, mechi ngumu yenye hadhi ya kuwa fainali, tumeshinda ugenini lakini kikanuni hatukufanikiwa, mabao ni 2-2, lakini tumeukosa ubingwa, tulikuja hapa kutafuta ushindi, tumeupata lakini haukutosha, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wachezaji wetu, benchi la ufundi na viongozi wote waliosafiri na timu, tumefanya kitu kikubwa hapa, haikuwa fainali ya mchezo, hata hivyo ni sisi tunajivunia tumefika fainali, sasa tunakwenda nyumbani kupokea ubingwa wetu wa ligi na kucheza fainali ya Kombe la FA, alisema Hersi.

# Simba yatuma ofa Al Hilal

INATOKA UK. 24

paja.

Mmoja wa 'Kigogo' wa bodi ya wakurugenzi wa klabu hiyo, alisema wanahitaji huduma ya wachezaji hao na tayari ofa iko mezani kwa vigogo hao wa Sudan.

Alisema wanaimani kubwa na kupata wachezaji hao kwa sababu ya ukaribu na urafiki uliopo kati ya Simba na klabu ya Al Hilal ambao wapo tayari kusikiliza ofa.

"Al Hilal wapo tayari kusikiliza ofa na kukaa meza moja kujadiliana kutokana na urafiki wa dhati uliopo kati yetu, kikubwa tunahitaji kuimarisha kikosi cha timu yetu kwa msimu ujao, tumedhamiria kufanya vizuri," alisema kiongozi huyo ambaye hakutaka jina lake liwekwe wazi.

Aliongeza kuwa wanaimani kubwa ya kupata huduma ya nyota hao kulingana na mahitaji ya timu yao kuelekea msimu ujao wa mashindano yatakayofanyika.

Aidha kwa upande wake, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kuhusu usajili msimu huu kila kitu kipo tayari na anaamini itakuwa na mwendo mzuri msimu ujao kwa kuwa inapata wachezaji wenye ubora kila idara.

"Kuhusu nani anasajiliwa hili jambo litawekwa wazi hapo baadaye na tayari kuna majina tunayo mezani kazi iliyopo ni mazungumzo, mashabiki wanapaswa kutulia na kujiandaa na msimu ujao kwani itakuwa timu kubwa na bora," alisema meneja huyo.

Simba kwa sasa inafanya maandalizi kwa ajili ya mchezo ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania unaotarajiwa kuchezwa Uwanja wa Azam Complex Juni 6.



Makabi Lilepo

# Michezo

Jumatatu Juni 5, 2023

Nipashe




**Ramos rasmi kuondoka PSG**

UKURASA 21



Rais wa Klabu ya Yanga, Hersi Said, akimkumbatia Nahodha wa klabu hiyo, Bakari Mwamnyeto, kabla ya kuvalishwa medali ya ushindi wa pili wa Kombe la Shirikisho Afrika juzi jijini Algers, Algeria. **PICHA: BINZUBERY**

# YANGA HAOO IKULU

## ●●●Injinia Hersi atoa medali kwa Rais, asifu jitihada zake kuinua michezo nchini, awapongeza wachezaji...

**Na Adam Fungamwango**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amealika wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa Yanga kwenye chakula cha jioni leo Ikulu, Dar es Salaam kwa lengo la kuipongeza kwa kufanya vizuri kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika iliyotamatika juzi.

Licha ya Yanga kuukosa ubingwa, ilipambana ugenini na kufanikiwa kushinda kwa bao 1-0 na hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa 2-2 baada ya awali Mei 28 kukubali kipigo cha mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Katika taarifa yake, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema Rais Samia amewapongeza Yanga kwa kucheza vizuri katika mchezo wa pili wa fainali wakiwa ugenini.

Msigwa amebainisha kuwa pamoja na kutotwaa ubingwa, Rais Samia anatambua kuwa Yanga imeipa heshima kubwa Tanzania na akawapongeza wachezaji wa timu hiyo ambao ni Mabingwa wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara.

"Timu ya Yanga, viongozi na mashabiki wanatarajia kurejea hapa nchini baadaye leo (jana) kwa ndege iliyotolewa na Rais, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono timu hiyo iliyokuwa ikiiwakilisha Tanzania kwenye mashindano hayo ya kimataifa, Rais anatambua jitihada za klabu hii hivyo amewaalika Ikulu ili kuwapongeza," ilisema taarifa hiyo.

INAENDELEA UK. 23

# Simba yatuma ofa Al Hilal

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umetuma rasmi maombi kwenye klabu ya Al Hilal ya kutaka kuwasajili wachezaji wawili wa timu hiyo ya Sudan.

Simba imetuma maombi ya kutaka kuwasajili golikipa wa timu hiyo, Issa Fontana, pamoja na mshambuliaji raia wa DRC, Makabi Lilepo ambaye anatajwa kuja kuchukua nafasi ya Augustine Okrah ambaye amepewa mkono wa kwa heri baada ya msimu huu kumalizika.

Simba imetuma ombi la kumsajili golikipa Fontana kwa ajili ya kuziba nafasi ya kipa namba moja wa timu hiyo, Aishi Manura ambaye atakuwa nje ya uwanja kwa miezi minne akiuguza jeraha baada ya hivi karibuni kufanyiwa upasuaji wa nyama za

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >